



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA KWANZA
JE! MANABII NI NANI?

MASOMO YA BIBLIA: Yermia
1:4-8; 2 Petro 1:20-21

Je! ni watu gani wanaoitwa manabii?
Je! kwa nini Mungu alichagua watu
fulani ili waweze kunena kwa niaba
yake wakati fulani au mahali fulani?

Utaweza kupata majibu ya maswali
haya na mengine mengi unapoendelea
kujifunza masomo haya kwa muda wa
miezi mitatu ijayo. Kila somo linahusu
mtu wa ajabu sana aitwaye nabii.

JE! NABII NI NANI?

Nabii wa kweli ni yule anenaye kwa
niaba ya Mungu. Watu wengi hudhani
kwamba nabii ni yule mtu awezaye
kusema jambo ambalo litafanyika
wakati ujao. Hii haikuwa ndiyo kazi
kuu ya manabii wa Kiebrania. Wakati
nabii aliponena alikuwa akiwaeleza
watu mapenzi ya Mungu. Hakusema
yale anayofikiria mwenyewe. Alisema
ujumbe wa Mungu aliyemwita na
kumpa maneno ya kusema.



Ukisoma Yermia 1:4-8, utaona jinsi
Mungu alivyomwita nabii huyu mkuu.
Nabii anaweza kuitwa “mtabiri” kwa
sababu aliweza kusema jinsi Mungu
alivyowafikiria watu wake na vitendo
vyao.

Ni kweli kwamba nabii aliweza kusema yale ambayo yangefanyika iwapo watu wangesikia na kutii Neno la Mungu au iwapo walitotii Neno lake. Hapa ndipo nabii anapoweza kuitwa “mtabiri.”

Jifanye kama kwamba ni lazima umwelezee mtu fulani kwamba nabii ni nani. Andika katika mistari ifuatayo yale ambayo ungemwambia mtu huyo.

JE! NABII HUPATAJE NENO LA MUNGU?

Manabii ambao tutajifunza habari zao ni watu ambao walimfahamu Mungu. Waliamini kwamba Mungu alikuwa akitawala kila jambo hapa duniani. Walimwamini Mungu na wakamtarajia kusema nao. Soma 2 Petro 1:20-21. Vifungu hivi vinatuambia kwamba manabii hawakusema ujumbe wao wenyewe. Roho Mtakatifu ndiye aliyewaletea ujumbe wa Mungu. Kusudi la kuhubiri kwao lilikuwa ni kuwasaidia watu wao kufahamu Mungu.

Kulikuwa na watu wengine ambao ni lazima tuwaite “manabii wa uwongo.” Dini zingine zilikuwa na watu ambao waliwashauri watu wao na kuwaambia yale ambayo yatatokea wakati ujao. Wengi wao walitumia uganga. Hawakumfahamu Mungu wa kweli na kwa hivyo hangeweza kusema ujumbe wa Mungu.

Kulikuwa na manabii wa uongo katika Israeli waliosema tu yale ambao watu walitaka wasikie. Haja yao ilikuwa ni kupata pesa na kuwapendeza watu. Manabii wa kweli wa Israeli hawakukubaliana na watu hawa.

JE! MANABII WALIHUBIRI KUHUSU NINI?

Manabii wa Mungu hawakuhubiri mahubiri marefu juu mambo ambayo watu hawakuyaelewa. Walizungumzia juu ya dhambi za watu. Waliona uongo na ukatili kuwa ni dhambi mbaya sana. Waliwatetea wajane na maskini. Walizungumzia juu ya hukumu ya Mungu kwa mahakimu waovu na wafanyakazi wavivu. Walikasirishwa sana na wale watu ambao walimwasi

Mungu na kuabudu miungu. Walizungumzia juu ya maangamizi ambayo yangetokea iwapo watu hao hawakumrudia Mungu.

Hata hivyo, manabii waliweza pia kutoa ujumbe wa tumaini. Walizungumzia juu ya upendo wa Mungu. Walisema kwamba, “Mungu yungali anatawala.” Walidhihirisha wazi kwamba Mungu hakuwa amewasahau watu wake, lakini atakuja kuwabariki siku moja. Naye angewatumia ili waubariki ulimwengu wote. Walihubiri kwamba Mungu angemtuma mfalme ambaye atakuwa mkuu kuliko Daudi na wa ajabu kuliko Sulemani. Mfalme huyu angetawala milele na milele.

JE! MANABII WALIISHI WAKATI GANI?

Manabii wa Kiebrania waliishi baada ya utawala wa Daudi na Sulemani. Hebu kwanza fikiria kwa muda wa

dakika moja yale yote uliyojifunza juu ya Waebrania. Kumbuka kwamba Musa aliwaongoza watu wa Mungu kule jangwani kwa muda wa miaka arobaini kabla ya kuifikia na kuisha katika nchi ya ahadi - Kanaani. Mungu aliwapa watu wa kuwaongoza alipokuwa akiwafanya kuwa taifa. Watu kama Yoshua walisaidia watu kujua kwamba Mungu alikuwa amewapa nchi ya ahadi Kanaani. Watu walipaswa tu kumwabudu Mungu Pekee. Walitakiwa kutii agano walilopewa na Mungu. Watu wajulikanao kama waamuzi walisaidia katika kuongoza taifa hili. Kulikuwa pia na makuhani ambao waliongoza ibada yao.

Samweli alitumiwa na Mungu kwa kazi kuu mbalimbali. Angekuwa kama mwamuzi, kuhani na nabii. Aliwaambia watu watubu dhambi zao na wamfuate Mungu wa kweli. Watu walitaka wawe na mfalme wa kuwaongoza kama mataifa yaliyojirani, wakati huu wa uongozi wa Samweli. Sauli alichaguliwa kama mfalme wa kwanza. Baadaye Daudi alifanywa mfalme halafu Sulemani akamfuatia. Kulingana na enzi za Sauli, mtu angefanywa mfalme kwa sababu baba yake alikuwa mfalme. Ni katika wakati huu ambapo Mungu alianza kuwaita manabii ili wanene kwa niaba yake.

Hatujui hasa wakati ule ambao watu hawa wote walinena ujumbe wa Mungu. Lakini, ujumbe wao uliweza kuandikwa na nabii mwenyewe au na mtu mwingine. Orodha ifuatayo itakusaidia kuelewa wakati ambao manabii hawa waliishi na kuhubiri. (Herufi hizi B.C. zinamaanisha Kabla ya Kristo.)


Miaka ya Biblia	Viongozi na Wafalme	Manabii
1800 B.C.	Ibrahimu (miaka na tarehe kamili haijulikani) Isaka	
1300-1200 B.C.	Musa, Haruni, Miriamu, Yoshua, Kalebu	
1020-922 B.C.	(Ufalme wa pamoja) Sauli, Daudi, Sulemani	Nathani, Eliya, Elisha
922-722 B.C.	(Ufalme uliogawanyika) Kulikuwa na Wafalme tofauti katika Yuda na Israeli	Yona, Amosi, Isaya, Mika, Hosea
722-587 B.C.	(Israeli ilishindwa mnamo mwaka wa 721 B.C.) Wafalme wa Yuda	Zefania, Nahumu, Habakuki, Yereimia
587-400 B.C.	(Yuda ilishindwa mnamo mwaka wa 587 B.C.) Zerebabeli, Nehemia, Ezra	Danieli, Ezeieli, Hagai, Zekaria, Obadia, Malaki
400-6 B.C.	Makabusi, Mfalme Herode	Yoeli
6-4 B.C.	Mfalme Herode	

KAZI YA KUFANYA

Andika herufi ya K kando ya sentensi iliyo ya kweli na herufi ya L kando ya sentensi isiyo kweli.

1. ——— Nabii wa kweli alikuwa yule aliyenena ujumbe wa Mungu.
2. ——— Manabii wengi wa Kiebrania waliishi baada ya kuzaliwa kwa Yesu.
3. ——— Mungu aliwachagua wafalme wote wa Israeli na Yuda.
4. ——— Kulikuwa na manabii wa uongo wa Kiebrania waliosema yale ambayo watu walipenda kusikiliza.
5. ——— Manabii wa kweli wa Kiebrania waliwahubiria watu juu ya hukumu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zao.

Hebu tazama katika orodha ifuatayo ya vitabu. Utaweza kuona majina yote ya vitabu vya Biblia. Je! ni vitabu vingapi? _____



Orodha ya vitabu vilivyoko katikati ni ya manabii. Vitabu vitano vilivyoko upande wa kushoto ni vya manabii

wakubwa, na vile kumi na viwili vilivyoko kwenye upande wa kulia ni vya manabii wadogo. Tofauti hii haipo kwa sababu ya umuhimu wao, bali ni kwa sababu ya ukubwa wa vitabu hivyo.

Kulikuwepo na watu wengine katika Agano la Kale ambao walijulikana kama “manabii hapo awali”. Hakuna vitabu ambavyo vinavyo majina yao. Lakini tunaweza kusoma habari zao katika vitabu vya historia. Tutajifunza juu ya mmoja wapo wa watu hawa aitwaye Eliya, katika somo lifuatalo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii...”
(Waebrania 1:1).

Utajifunza jinsi Mungu alivyonena na yale aliyosema kupitia kwa manabii, kwa muda wa wiki kumi na mbili zijazo. Ujumbe huu ulitolewa kwa watu miaka mingi iliyopita, lakini ni wa muhimu kwetu hata leo. Maovu mengi yaliyokuweco siku hizo yangaliko hata wa leo.

Jiahidi wewe mwenyewe kwamba utajifunza masomo haya kwa uangalifu. Utafurahi sana kupata kujua watu hawa waitwao manabii. Nawe utajifunza mengi zaidi jinsi Mungu atakavyo watu wake waishi siku hizi.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA PILI

ELIYA, NABII MWENYE UJASIRI

MASOMO YA BIBLIA: 1 Wafalme 17:1; 18:1-2, 20-24, 36-39


Je! Unajifunza majina ya vitabu vya manabii? Ikiwa unajifunza utaona kwamba nabii unayejifunza habari zake leo hakuandika kitabu cho chote. Hata hivyo, watu wengine waliweza kuandika juu ya nabii Eliya. Unaweza kusoma jinsi Mungu alivyomtumia Eliya katika 1 Wafalme 17 hadi 2 Wafalme 2.

JE! ELIYA ALIKUWA NANI?

Hebu tumsikilize Eliya jinsi anavyojitambulisha mwenyewe. "Jina langu ni Eliya. Niliishi wakati wa miaka mia moja iliyopita, kabla ya Amosi. Mungu alinitumia kama nabii katika ufalme wa Kaskazini wa Israeli kwa muda wa miaka hamsini baada ya kifo cha Sulemani. Ukitazama ramani ifuatayo utaona kwamba mji mkuu wa nchi yangu ulikuwa Samaria."



Dunia ya Manabii



"Niliishi wakati Ahabu alipokuwa mfalme wa Israeli. Ahabu na malkia wake, Yezebel, walikuwa wamewaleta manabii wengi wa uongo nchini Israeli.

Manabii hawa walikuwa wakiwaongoza watu katika uabuduiji wa mungu uitwao Baali. Malkia Yezebeli alikuwa ameamuru kuuawa kwa makuhani wa Mungu Yehova. Alikuwa akimwabudu Baal tangu hapo zamani na akataka kuwaongoza watu katika kuabudu mungu huu wake.

“Waisraeli walianza kufikiri kwamba ilikuwa vyema kwenda katika hekalu la Baali lililoko Samaria. Pia, lile hekalu lililokuwa Yerusalemu lilikuwa mbali sana. Watu hawa walichanganyikiwa na mawazo na wakaanza kumwabudu Baali, pamoja na Mungu wa kweli, Yehova.

“Mungu aliniambia kwamba ni lazima niwakanye kutoabudu Baali. Nilijua kwamba Ahabu na Yezebeli walitaka kuniua, lakini Mungu alinipa ujasiri wa kunena kwa niaba yake.”

ELIYA ANENA KWA UJASIRI

Umemsikia Eliya akieleza jinsi hali ilivyokuwa kule Israeli. Mungu hakupendezwa na matendo ya watu wake, kwa hivyo alimwambia Eliya awakanye juu ya kuabudu Baali. Eliya angenyamaza tu kwa sababu ya woga, lakini aliamini kwamba Mungu atamlinda.

Eliya aliponena kwa niaba ya Mungu alisema kwamba hakungekuwa na mvua wala umande kwa muda mrefu sana. Mungu aliweza kumtimizia Eliya hitaji la chakula na maji wakati huu wa ukame mkuu.

Baada ya miaka mitatu kupita Mungu alimtumia Eliya kwenda kwa Mfalme Ahabu na kusema naye kwa sababu alikuwa tayari kunyesha myua. Ahabu alikuwa akimtafuta sana Eliya,

kwani yeye na Yezebeli walikuwa wanataka wamwue.

Wakati Ahabu alipomwona Eliya, alimlaumu kwa kusababisha shida iliyokuwa Israeli. Eliya akamjibu, “Sijasababisha shida ye yote. Wewe mwenyewe unapaswa kulaumiwa kwa sababu umekataa kutii amri za Mungu. Hasa umeabudu sanamu ya Baali.”

Eliya aliendelea kusema kwamba yeye ndiye aliyekuwa mfalme badala ya Ahabu. “Nataka utoe ujumbe kwa Israeli yote,” akaamuru. “Waambie wakutane nami katika mlima wa Karmeli. Waletе pia wale manabii mia nne na hamsini wa Baali na wale manabii mia nne ambao hula pamoja na Malkia Yezebeli.”

Hapakuwa na nyasi chakula cha ng’ombe. Mito ilikuwa imekauka na hapakuwa na chakula nchini mwote. Mfalme Ahabu alikuwa tayari kufanya cho chote atakachoambiwa. Alifanya jinsi Eliya alivyoeamuru. Watu walikusanyika karibu na mlima wa Karmeli.

NI LAZIMA WATU WAAMUE CHA KUFANYA

Eliya aliwaambia watu wafanye uchaguo watakao. Soma 1 Wafalme 18:21 uone ni uchaguo upi walioambiwa.

Eliya alijua kwamba kutoabudu kwa watu kwa Mungu wa kweli ndiko kuliolitaabisha taifa hili. Alikuwa na mpango wa kuwasaidia watu kuamua ni yupi aliyekuwa Mungu wa kweli. Soma 1 Wafalme 18:23-24 ili ujue mpango wa Eliya.

Manabii wa Baali ndio walioanza. Walichagua ng’ombe mmoja wa kutoa

dhahibu na wakamweka madhabahuni. Walimwomba na kumsihi Baali awalettee moto wa kuchoma dhahibu yao.



Je! jambo lo lote lilitokea? Soma 1 Wafalme 18:26 ili upate jibu.

“Mwiteni na kuomba kwa sauti kuu,” Eliya akawafanyia dhahika. “Labda mungu wenu analala au amesafiri,” Eliya akawaambia.

Ilipotimia mwendo wa saa tisa adhuhuri, Eliya alianza kutengeneza madhabahu ya kutolea dhahibu yake kwa sababu wale manabii wa Baali hawakufanikiwa kamwe. Eliya alifanya mambo mengi kabla ya kuomba. Soma 1 Wafalme 18:31-35 ili uone jinsi alivyojitayarisha. Eliya aliwaambia waimwagie sadaka hiyo maji kutoka kwa mapipa manne mara tatu. Haikosi kuwa watu walifikiria kwamba sadaka wala kuni hizo hazingeshika moto.

Eliya aliomba ombi fupi sana. Ombi hili lapatikana katika 1 Wafalme 18:36-37.

Mungu alijibu ombi hili? Soma kifungu cha 38. Watu walianguka kifudufudi walipoona yaliyotokea. Wakasema, “Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu.”

Eliya aliwaambia kwamba ikiwa wanaamini yale wanayosema, watatakiwa kuwaangamiza manabii waliowaongoza katika uovu. Akamwambia Ahabu ainuke ale na anywe kwa sababu itanyesha mvua.

JE! WAZEWA KUJIFUNZA NINI KUTOKA KWA ELIYA?

Eliya alisema ukweli ambao Mungu alitaka watu wake wasikie. Alizungumza kwa ujasiri juu ya dhambi za Mfalme Ahabu. Eliya alihitaji ujasiri mkuu sana ili kuongea hivyo mbele ya mfalme wa Israeli.


Eliya hakutenda yaliyomema kwa uwezo wake mwenyewe. Alimwamini Mungu. Mungu alimpa Eliya nguvu za kusema kwa ujasiri.

Je! kuna wakati ambapo unapaswa kusema ukweli lakini waona shida kuusema? Maisha ya Kikristo si rahisi. Lakini Mungu atakupata ujasiri wa kuishi kwa ajili yake iwapo utamwamini.

KAZI YA KUFANYA

Je! unapenda michezo? Hapo chini kuna mchezo mpya. Mwalimu wako atakusaidia iwapo utapata shida ya kutafuta majibu yake.

Soma kila maandiko uliyopewa. Tafuta jibu la swali hilo katika kifungu ulichopewa. Sasa tafuta jibu lake katika fumbo la maneno uliyopewa. Utapata jibu lake kwa kusoma ukielekea chini, kulia au kutoka kwa pembe hadi pembe nyingine. Sasa chora mviringo kwa neno hilo. Umepewa jibu la kwanza kama mfano wa kukuonyesha jinsi ya kufanya.



1. Soma 1 Wafalme 18:1. Je! Mungu alinena na nani? Jina lake linaanza na herufi E.
2. Soma 1 Wafalme 18:2. Je! Ni mfalme yupi aliyemchukia Eliya? Jina lake linaanza na A.
3. Soma 1 Wafalme 18:20. Je! Eliya aliwaambia watu wakutanike kwa mlima gani? Jina lake linaanza na herufi ya K.
4. Soma 1 Wafalme 18:22-24. Je! Manabii wale walihudumia mungu upi? Jina la mungu huo linaanza na herufi ya B.
5. Soma 1 Wafalme 18:25. Je! Wale waongozi wa uongo wa dini waliitwaje? Jina lao linaanza na herufi ya M.
6. Soma 1 Wafalme 18:25. Je! Mahali ambapo Eliya alitengeneza pa kutolea sadaka paliitwaje? Jina lake linaanza na herufi ya M.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho, zaidi yangu mimi hapana Mungu" (Isaya 44:6b).

Eliya alimwamini Mungu naye akampa ujasiri wa kusema ukweli. Alijua kwamba lilikuwa jambo la muhimu kwa Waisraeli kuacha kuabudu sanamu. Je! Una ujasiri wa kusimama imara kwa ajili ya Mungu wa kweli? Unaweza kupatwa na shida fulani. Kwa mfano, inaweza kuwa ni wewe tu katika darasa lenu ambaye hapendi kudanganya. Je! utamruhusu Mungu akupe ujasiri wa kusema ukweli?

Kifungu chako cha kukumbuka kimeandikwa hapo chini bila herufi kadhaa. Andika herufi zilizoachwa mahali panapotakikana na ukamilishe usemi huu wa Mungu.

M _ M _ N _ W _ KW _ NZ _
N _ M _ M _ N _ W _ MW _ SH _
Z _ J _ Y _ NG _ M _ M _
H _ P _ N _ M _ NG _

Isaya 44:6b



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA TATU

AMOSI AHUBIRI JUU YA HUKUMU YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Amosi 1:1-2;
2:4-8; 8:11-12

Sisi sote hupenda kusikia juu ya upendo na ulinzi wa Mungu kwetu. Wachache kati yetu hupenda kuambiwa kwamba tutaadhibiwa kwa makosa tuliyofanya. Hivi ndivyo ilivyokuwa kulingana na watu wa wakati wa Amosi. Mungu hutukanya wakati ambapo hatufuati njia yake kwa sababu anatupenda. Mungu aliwapenda watu wa Yuda na Israeli. Alitaka kuwaonya juu ya yale ambayo yangewapata iwapo hawakuirudia njia yake. Kwa hivyo, alimwita Amosi ili amnencee.

Hebu, jifanye kama kwamba unasikiliza redio. Fikiria kwamba watu walikuwa na redio mnamo miaka mia nne kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Naye mwandishi wa habari ametoka katika nchi yako ili ahojiane na Amos na wale watu wa wakati wake. Hebu sikiliza yale wanayosema.

Mwandishi: Hamjambo nyote. Huyu ni msimulizi wenu wa habari wa Agano

la Kale anayezungumza nanyi kupitia kwa Sauti ya Yerusalemu. Niko hapa katika Ufalme wa Kusini wa Yuda. Nchi hii inaendelea vizuri kwa kila jambo. Watu wengi wa hapa wameendelea sana na nchi yenyewe ina jeshi hodari sana. Ila tu naona kwamba kuna tatizo moja hapa. Mchungaji kondoo na mkuzaji mitini atokaye katika kijiji cha Tekoa ambacho ni umbali wa kilomita kumi na sita kutoka Yerusalemu, anahubiri mahali paitwapo Betheli palioko karibu na hapa nilipo. Watu hawapendi yale asemayo.

Kwa sasa ninaongea na watu wapitao katika njia za mji huu ili nisikie maoni yao juu ya Amosi. Mtu huyu anayekuja sasa anaonekana kama anaweza kutuambia jambo fulani.

Mwandishi: Habari yako?

Mtu wa 1: Nzuri sana

Mwandishi: Je! unafikiriaje juu ya Amosi ambaye anazusha fujo hapa Yerusalemu?

Mtu wa 1: Aha! Unamaanisha yule mchungu-kondoo atokaye Tekoa? Amekuwa akimkanya kila mmoja wetu ya uharibifu utakaotokea Yuda na mataifa mengine yaliyo karibu nasi. Alisema kwamba watu wa Yuda wamesahau kumwabudu na kumtumikia Bwana. Hata alisema kwamba wao ni waongo. Hata sielewi kwa nini anazungumza hivyo juu ya watu wake.

Mwandishi: Umetaja pia hata nchi zingine. Je! ni nchi gani hizi?

Mtu wa 1: Amosi mhubiri, alisema kwamba Mungu ataiadhibu nchi ya Gaza, Tiro, Edomu, Moabu, na Yuda. Halafu akaanza kuongea juu ya Israeli, ambayo ni Ufalme wa Kaskazini. Sidhani kama watu huko watafurahi watakaposikia hivyo. Hata hivyo, Amosi mwenyewe anatoka Yuda. Hajui cho chote juu ya Israeli!

Mwandishi: Nadhani tutangojea tu na tuone kile kitakachotokea. Asante sana kwa maoni yako.

Mtu wa 1: Nimeshukuru sana. Hata nimefurahi kukwambia yale nijuayo.

Mwandishi: Umeshasikia maoni ya mmojawapo wa wenyeji wa Yuda. Jana nilikutana na mwanamke mmoja ambaye amehudhuria sana mahubiri ya Amosi. Rachel Moses yuko nami leo. Rachel unaweza kutwambia yale uliyosikia?

Rachel: Kwa kweli nimeona kwamba mtindo wa Amosi wa kuanza kuhubiri ni ule ule tu wa mwanzo. Huanza kwa kusema, "Haya ndiyo asemayo Bwana, kwa makosa matatu ya..." Halafu akataja zile nchi anazoongea juu yake. Akaendelea hivi, "...naam, kwa manne, sitaizua adhabu yake isimpate..." Hatimaye

akataja dhambi zilizotendwa na nchi hiyo.

Mwandishi: Nimesikia kwamba Amosi ameanza kuihukumu Israeli. Alisemaje juu ya dhambi zao?

Rachel: Alisema kwamba watu wa Israeli (nami nasema vile alivyosema) "...wamewauza wenye haki kwa fedha na maskini kwa jozi ya viatu." Alisema kwamba watu wao walikuwa wachoyo na walikuwa wamewadanganya maskini. Amosi alisema pia kwamba kulikuwa na dhambi ya uzinzi kila mahali.

Mwandishi: Je! matendo haya ambayo Amosi anayaita "dhambi", yana uhusiano wa wote na Mungu Yehova ambaye watu wanamwabudu?

Rachel: Amosi alisema kwamba matendo kama haya yanaonyesha kuwa watu hawamtii Mungu. Aliongezea kusema kwamba hata viongozi wa kidini wa wakuu wa serikali wana hatia ya dhambi hii. Watu wengi hata hawajali iwapo hawatii amri za Mungu.

Mwandishi: Je! Unafikiri mahubiri haya yataleta mabadiliko yo yote kwa watu wa Israeli?

Rachel: Sina uhakika. Hasa watu wanaonekana kama wametoshaka na jinsi mambo yalivyo. Uchumi wa nchi yao ni mzuri hata wana jeshi bora zaidi. Naamini kwamba watu wengi hawatafikiria kuwa wanapaswa kubadilisha matendo yao.

Mwandishi: Je! Amosi amewahi kulinganisha dhambi za Israeli na Yuda na zile za mataifa mengine?

Rachel: Alisema tu kwamba mataifa mengine yamewatendea watu dhambi. Lakini Yuda na Israeli wamemtendea Mungu dhambi kwa

sababu wanadai kwamba wana-mwabudu Mungu Yehova.

Mwandishi: Nimesikia kwamba Amosi anazungumzia sana juu ya hukumu ya Mungu kwa watu wote. Je! Unafikiri kwamba watu wanaiogopa hukumu ya Mungu?

Rachel: Inaonekana kwamba watu hawafikirii kama jambo lolote litafanyika kwao. Wameshangaa na kukasirika kwa sababu Amosi anafikiri kwamba wanapaswa kuhukumiwa na Mungu.

Mwandishi: Asante sana sana Rachel Moses kwa maoni yako. Umetusaidia sana kuweza kuelewa vyema yale yanayofanyika hapa kwenu. (Baada ya siku kadhaa kupita, Mwandishi wa habari wa Agano la Kale alirudi tena katika njia za mji wa Yerusalemu. Hebu tusikilize yale atakayo sema tena leo.)

Mwandishi: Jua limechomoza vizuri sana leo. Yerusalemu ni mji wenye shughuli nyingi. Mamia ya watu wanajishughulisha sana hasa na kazi zao na biashara. Sasa naweza kuelewa wazi jinsi ilivyo vigumu kwa watu kuamini kwamba wanaweza wakapatwa na hukumu ya Mungu. Hata hivyo, hakuna awezaye kubisha kwamba Amosi ni mhubiri mzuri. Anaongea kama kwamba ujumbe wake unatoka kwa Mungu.

Ngoja kidogo! Je! Ni nani huyu ambaye anatumia? Aha, ni Amosi. Hii ni siku ya bahati kwetu. Tutamsikia Amosi akiongea nasi.

Bwana Amosi, Je? Tunaweza kukuuliza maswali machache? Mazungumzo haya yanatangazwa hapa Afrika. Watu wanataka kujua sana kile kinachotendeka hapa.

Amosi: Ndiyo, ninazo dakika chache tu. Je! Ungependa kujua nini?

Mwandishi: Umekuwa ukihubiri sana. Je! Unaweza kutoa muhtasari wa ujumbe wako?

Amosi: Ndiyo, ninaweza. Ukweli ni kwamba ikiwa watu hawataanza kumtii Mungu, basi Mungu atawaacha wafanye jinsi watakavyo. Ataacha hata kusema nao.

Mwandishi: Je! Unadhani ni nini kiwezacho kutokea?

Amosi: Kwanza kabisa, watu hawatakosa Neno la Mungu. Lakini baadaye watataka kulisikia. Matokeo yake yatakuwa sawa na yale ya njaa. Wakikaa bila Neno la Mungu ndivyo watakavyosikia njaa ya kulisikiliza. Watamtetea Mungu ili ajidhihirishe kwao tena.

Mwandishi: Kutakuwa na hali mbaya sana!

Amosi: Ndiyo, inaweza kuwa hivyo iwapo watu watakataa kusikiliza mapema. Na ndiyo sababu niko hapa. Niliacha kondoo na kukuza mimea yangu ili niwaambie watu wa Yuda na Israeli. Ninataka kile ambacho Mungu anawatakiwa watu hawa. Anataka kuwaona wakiishi maisha ya furaha na amani. Watasamehewa tu iwapo wata-mrudia Mungu na kuishi kwa haki.

Mwandishi: Amosi, asante sana kwa kutumia dakika chache kwa kutueleza juu ya ujumbe wako. Ninaamini kwamba watu wataku-sikiliza.

Huyu ni mwandishi na msimulizi wenu wa Agano la Kale akisema

“Kwaherini” kwa leo. Nitakuwa nanyi tena kesho wakati kama huu pamoja na habari nyingine zaidi.

KAZI YA KUFANYA

Mungu alimwita Amosi ili azungumzie juu ya dhambi za Waisraeli. Alizungumzia pia dhambi za watu wake wa Yuda. Soma Amosi 2:4-8 na uandike orodha ya dhambi za Yuda na Israeli kwa maneno yako mwenyewe.

Dhambi za Yuda

Dhambi za Israeli

- | | |
|---------------------------------|--------------------------------------|
| —1. Tekoa | a. miaka ya huduma Amosi |
| —2. Yuda | b. kazi ya Amosi kabla ya kuwa nabii |
| —3. Israel | c. Ufalme wa Kusini |
| —4. Mchungaji na mkuzani mitini | d. Matokeo ya kumkataa Mungu |
| —5. Hukumu | e. mji mkuu wa nyumbani kwa Amosi |
| —6. 760-753 B.C. | f. Ufalme wa Kaskazini |

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

Amosi angesema maneno yale yale iwapo angewazungumzia vijana wa siku hizi. Andika katika nafasi ifuatayo aya moja ya ujumbe ambao unadhani Amosi angesema iwapo angekuwa bado yungali hai.

Soma Amosi 8:11-12. Vifungu hivi vinatoa mfano jinsi mambo yangekuwa kwa watu wa Israeli iwapo hawangetubu. Chora picha ambayo imesimuliwa katika Amosi 8:11-12 katika nafasi ifuatayo.

Kamilisha fungu la maneno lililoko upande wa kushoto na maelezo yaliyoko upande wa kulia kwa kuandika herufi ifaayo katika nafasi iliyoachwa.

“Tafuteni mema, wala si mabaya, mpate kushi; hivyo Bwana, Mungu wa Majeshi, atakuwa pamoja nanyi, kama msemavyo” (Amosi 5:14).

Amosi aliwaonya watu kwamba wakati unakuja ambapo hawatakuwa na Neno la Mungu iwapo wataendelea na dhambi zao. Mungu hakutaka jambo hili litokee. Hii ndiyo sababu iliyomfanya amtume Amosi ili awaonye.

Mungu anakupenda jinsi alivyo-wapenda watu wake hapo kale. Hata hivyo, hawezi kukuacha utende dhambi. Je! Kuna kitu maishani mwako ambacho kinakutenganisha na Mungu? Je! Unataka ufanyeje juu ya jambo hili?



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU **KITABU CHA PILI**

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA NNE
HOSEA ANAELEZA UPENDO WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Hosea 11:1-4;
14:1-4

Maria alisikitika sana kwa siku
kadhaa. Alikuwa amesema uongo juu

ya Prisila. Sasa alijua kwamba ni lazima
amwende Prisila na amwombe
msamaha.



"Prisila, Je! Naweza kusema nawe kwa dakika moja tu?"

"Juu ya nini?" Prisila akamjibu mara moja.

"Wewe unajua baadhi ya mambo niliyosema juu yako." Maria alianza kutoka machozi. "Hata sikujua kwamba haya yote yangetokea. Nilikuwa tu na wivu kwa sababu wewe huwa wa kwanza katika kila jambo pale shuleni. Hata hivyo, nisingeweza kuzuia uvumi ambao niliuanzisha pale shuleni. Kwa hivyo nimekuja kukuomba msamaha. Je! Utanisamehe?"

Prisila alimwalia Maria na macho ya chuki. "Sitakusamehe kamwe," alimwambia alipoanza kwenda zake.

Pengine umewahi kupatwa na mkasa kama huu. Je! Uliweza kudhani kwamba huwezi kumwomba Mungu msamaha?

Utajifunza kutoka kwa nabii Hosea kwamba Mungu huitikia kwa njia tofauti na ile ya Prisila.

Tangu ulipoanza somo hili la manabii umejifunza na kusikia mengi juu ya dhambi za Israeli na Yuda. Manabii hawa hawakuogopa kuwaambia watu jinsi Mungu angewahukumu kutokana na dhambi zao. Hosea pia, alizungumza juu ya hukumu. Lakini ujumbe wa Hosea ni tofauti kwa sababu alizungumza zaidi juu ya upendo wa Mungu kwa watu wake. Alisema kwamba Mungu angewasamehe wote ambao watatubu.

Hosea alijua maana ya kusamehe. Alikuwa na mke asiyemwaminifu aitwaye Gomeri. Alijiaibisha yeye

mwenyewe pamoja na jamaa yake. Lakini Mungu alimwambia Hosea amchukue tena mkewe na amsamehe. Jambo hili lilimfanya Mungu aweze kumtumia Hosea kwa kufundisha Israeli jinsi Mungu alivyowapenda watu wake. Aliweza kuifundisha Israeli jinsi alivyo na moyo wa kusamehe.

Hosea aliishi katika Ufalme wa Kaskazini mwa Israeli. Yeye alihubiri huko wakati Isaya alipohubiri katika Ufalme wa Kusini. Mungu alimtumia Hosea kwa kunena na watu wake kuanzia mwaka wa 748 B.C. hadi 722 B.C.

Soma Hosea 11:1-4. Je! Hosea alifananisha uhusiano wa Mungu na Israeli na nini? Andika jibu lako hapa.

_____ na _____
Je! Uliandika baba na mwana katika nafasi ilioachwa?

Mungu alikuwa amewaita watu wa Israeli wamfuata. Alitaka awatumie ili auonyeshe ulimwengu jinsi alivyo. Hatimaye alifanya agano nao. Mungu aliwaokoa kutoka utumwani kule Misri na akawaongoza hadi katika Nchi ya Ahadi. Aliwakumbusha wakiwa huko juu ya agano alilofanya nao. Wote walikubali kumfuata na kumtii. Walimtii Mungu kwa muda mfupi hatimaye walimsahau na wakaanza kuabudu miungu.

Mungu aliendelea kuwapenda hata ingawa walikuwa kama mtoto aliyeasi. Aliwataka wamrudie. Sababu moja iliyomfanya awatume manabii kama Hosea ilikuwa ni kuwaonya juu ya matokeo ya dhambi zao.

Picha ambayo imeelezwa katika kifungu cha nne inaonekana zaidi kama

ya ng'ombe kuliko ya mtoto. Hata hivyo, Hosea alikuwa akisema kwamba Mungu alikuwa tayari kutimiza mahitaji ya watoto wake. Mungu alitoa malezi na miongozo kwa Waisraeli. Aliwapatia pia chakula cha kiroho na kimwili.

Israeli ilikuwa kama mtoto ambaye hafikirii. Watu walimdharau Mungu. Hawakuonyesha kama walijua au kujali kwamba baraka zao zinatoka kwa Mungu. Hata hivyo Mungu aliwapenda na alikuwa akiwangoja ili awakaribishe tena kwake.

Sasa soma Hosea 14:1-4. Je! Unakumbuka hadithi uliyosimuliwa katika mwanzo wa somo hili? Maria alipopata ujasiri wa kuomba msamaha, Prisila alikataa kumsamehe. Mungu si kama Prisila. Usiógope kukiri dhambi zako mbele ya Mungu. Yeye yuko tayari kumsamehe mtu ye yote ambaye atatubu dhambi zake kwa moyo wa kweli.

Hosea, katika vifungu hivi anasema kwamba Mungu yu tayari kuisamehe Israeli. Lakini Israeli nayo inayo wajibu. Hebu tazama maneno ya kifungu cha 1, "Ee, Israeli, mrudie Bwana Mungu wako." Mungu atawasamehe wale watakaomrudia au kutubu dhambi zao na kuomba msamaha.

Kwa hivyo jambo la kwanza ambalo ni lazima ufanye ili usamehewe ni kukiri dhambi zako kwa moyo wa kweli na kumwomba Mungu msamaha. Usifikirie kwamba dhambi zako ni kubwa sana ambazo Mungu hawezi kuzisamehe. Upendo wake ni mkuu zaidi kuliko dhambi zako.

Wakati mtu anapokiri na "kusikitika" dhambi zake, ni lazima awe anasema kwa moyo wa kweli. Halafu awe tayari kubadili matendo yake.

Mungu aliwapa watu wake miongozo hiyo hiyo alionena na Israeli kupitia kwa nabii wake Hosea. Aliwaambia waache kuabudu sanamu na wamfuate kwa maneno na matendo. Aliwaambia kwamba haijalishi yale ambayo wametenda kwani yungali anawapenda na yuko tayari kuwasamehe. Aliendelea kutafuta njia za kuonyesha huruma wema na upendo wake.

KAZI YA KUFANYA

Jaza nafasi iliyoachwa kwa kutumia maneno au usemi ulioko katika orodha iliyo chini ya sentensi zifuatazo:

1. Hosea alikuwa nabii wa _____

2. Mkewe Hosea alikuwa akiitwa _____

3. Israeli ilitenda kama _____ aliyeasi na kukosa kutii.
4. Mungu _____ Israeli bila kutojali dhambi zake.
5. Ni lazima Israeli _____ Bwana ili Mungu aweze kuisamehe.

(Mtoto, Gomeri, Imrudie, Ufalme wa Kaskazini, aliipenda)

Somo hili limekusaidia kuelewa kwamba Mungu anawapenda na atawasamehe watoto wake. Anawapenda wale wanaomtii, lakini anawapenda pia wale ambao wamemwasi. Hii haimaanishi kwamba

Mungu hakuhuzunika wala kuudhika tunapotenda dhambi. Dhambi ni kitu kibaya sana naye Mungu huteseka tunapoitenda. Lakini, Mungu ni mwenye huruma na yuko tayari kutusamehe.

Je! Kuna dhambi maishani mwako ambayo unataka Mungu akusamehe? Basi ni lazima ukiri kwa kweli dhambi hiyo, ukubali kwamba unayo dhambi na uombe msamaha. Haupaswi kubeba mzigo wa dhambi hizo, kwa sababu Yesu alijitwika mzigo wa dhambi zako. Tumia dakika chache kufanya mambo yafuatayo:

1. Mwombe Mungu akuonyeshe dhambi ulizonazo.
2. Andika kwenye karatasi dhambi hizi zote ambazo hujaomba usamehewe.
3. Kiri kila mojawapo ya dhambi hizi.
4. Mwombe Mungu akusamehe na akutendee mema katika sehemu hizi ulizotaja.
5. Sasa zitupe karatasi hizi. Mungu ameshakuondolea dhambi hizi iwapo ulitubu kwa moyo wa kweli. Hata nawe waweza kufanya hivyo!
6. Sasa uko tayari kumwonyesha Mungu upendo wako kwa kumtii.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, na dhambi zao sitazikumbuka tena" (Waebrania 8:12).

Hakuna mtu ambaye angemlaumu Mungu iwapo angewaacha watu wake wa Israeli. Wao waliendelea kutomtii hata ingawa aliwaonya kupitia kwa manabii. Lakini ukweli ni kwamba Mungu hakufa moyo. Aliendelea

kutafuta njia za kuweza kuwaonyesha upendo na huruma zake. Mungu alionyesha upendo na huruma zake kwa kuiita Israeli kuwa taifa na kuwa mwaminifu kwao hata ingawa walikuwa wametenda dhambi. Mwishowe, wakati ulipotimia, Mungu aliweza kumtuma Mwanawe, Yesu Kristo, kuja ulimwenguni ili afe kwa ajili ya dhambi za watu wote. Kila mtu ambaye anamjia Kristo kwa moyo wa kutubu atasamehewa.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA TANO

ISAYA ALIITWA KUTOA HABARI NJEMA

**MASOMO YA BIBLIA: Isaya 6:1-8;
9:6-7**

Je! Umewahi kuwaza ni kwa nini wachungaji na watu wengine husoma sana maandiko ya kitabu cha Isaya wakati wa Krismasi? Hata ingawa Isaya alizaliwa karibu miaka 760 kabla ya Kristo, aliweza kuzungumza juu ya kuja kwake. Isaya alitwa kutoa ujumbe muhimu — habari ya kuzaliwa kwake Yesu Kristo.

Hata Wakristo wa siku hizi wanaitwa ili watoe habari muhimu sana. Wanaitwa ili wawaambie wenzao kwamba Yesu alikuja ili kutoa maisha mapya kwa kila mmoja hapa duniani.

Ulijifunza katika somo la kwanza kwamba Mungu ndiye aliyewaita manabii wa kweli. Utajifunza katika somo hili jinsi Mungu alivyomwita Isaya na kile alichomtaka afanye. Fikiria yale ambayo Mungu anakwita ufanye wakati unapoendelea kujifunza na kusoma somo hili.

Isaya alikuwa mtoto wa mtu aitwaye



Amozi. Alizaliwa Yerusalemu ambako alihubiri kwa muda wa miaka arobaini.

Isaya alijua mengi kuhusu historia na siasa. Aliishi wakati wa utawala wa wafalme wanne tofauti. Nao walikuwa Uzia, Yothamu, Ahazi na Hezekia.

Isaya aliuona pia uovu wa watu jinsi ilivyokuwa na manabii wengine. Alijua

kwamba Mungu angewaadhibu kwa kuwaacha watekwe na kupelekwa katika nchi nyingine kama wafungwa. Lakini watu wanapomfikiria Isaya, huwa hasa wanafikiria juu ya habari njema alizohubiri.

Aliwaambia watu mara kwa mara kwamba Mungu atamtuma yule aliyeahidiwa ambaye angewaokoa kutoka kwa dhambi zao. Sasa twajua wazi kwamba huyo alikuwa Yesu.

MUNGU ANAMWITA ISAYA

Mfalme Uzia alikuwa amefanikiwa sana. Alikuwa amesaidia kuleta amani kati ya watu. Watu waliogopa sana kwa yale ambayo yangetokea wakati Uzia alipokufa. Mwanawe Uzia, aitwaye Yothamu, alikuwa dhaifu na maadui wa Yuda walikuwa wakiendelea kuwa wenye nguvu.

Huu ulikuwa mwaka wa 742 B.C. naye Isaya alikuwa na umri wa miaka ishirini. Pengine aliwazia sana yale ambayo yangempata. Alienda Hekaluni na akaanza kuomba. Isaya aliota ndoto ya ajabu alipokuwa katika hekalu la Yerusalemu. Aliona vitu vya ajabu katika ndoto hiyo. Hakumwona Mungu, bali aliona pia viumbe vya ajabu katika ufalme wa Mungu.

Soma Isaya 6:1-4. Sasa jaza nafasi zilizoachwa kwa maneno yanayoeleza jinsi viumbe hivi vya mbinguni vilivyo.

1. Kiti cha Enzi cha Bwana kilikuwa _____ na kimeinuliwa sana. (kifungu cha 1)
2. Pindo la vazi la Bwana zilikuwa zimeijaza _____ (kifungu cha 1)
3. _____ walisimama juu ya Bwana (Kifungu cha 2).

4. Kila _____ alikuwa na _____ sita. Mawili yalifunika _____ wake. Mawili yalifunika _____ yake, na alitumia mengine mawili kwa _____. (Kifungu cha 2)

5. Waliitana na kuimba, _____, _____ ni Bwana wa majeshi. (Kifungu cha 3)

6. Sauti zao zilifanya _____ vya Hekalu vitisike nayo Hekalu ikajaa _____ (kifungu cha 4)

Je! Ungejisikiaje ikiwa ni wewe ambaye uliona vitu hivi vya ajabu? Isaya alijisikia kama yeye si kitu mbele za Mungu. Alijiona kama yeye si msafi na akakiri dhambi zake.

Soma Isaya 6:5-8. Lile kaa la moto lililotolewa kwenye madhahabu lilionyesha kwamba Mungu alimsamehe Isaya dhambi zake.

Isaya alijiona jinsi alivyo wakati alipoona jinsi Mungu alivyo mtakatifu. Alitubu dhambi zake. Mungu alimsamehe dhambi zake na akampa kazi ya kufanya. Mungu alimwita Isaya ili anene kwa niaba yake kwa watu wa Yuda. Alimhitaji mjumbe wa kuwakumbusha watu juu ya dhambi zao. Alihitaji mtu wa kuwaambia watu jinsi Mungu atawahurumia na kumtuma yule aliyeahidiwa.

Isaya alikubali kunena kwa niaba ya Mungu kwa ulimwengu ulio na hitaji kuu. Akasema, "Mimi hapa, nitume mimi."

Isaya alipoanza kuhubiri hakuacha kuwaambia watu juu ya hukumu ya Mungu. Aliongea na Wafalme lakini wote hawakusikiliza mashauri yake.

Isaya alileta ujumbe maalum sana ambao watu hawakuwa wamewahi kuusikia wakati huu wa siku za giza. Aliwaambia watu kwamba Bwana angemtuma yule aliyeahidiwa ambaye angewaokoa kutoka kwa dhambi zao. Huyu aliyeahidiwa angekuwa mfalme mkamilifu ambaye ufalme wake haungeisha.

Soma Isaya 9:6-7. Hapa chini kuna majina ambayo yamepewa huyu aliyeahidiwa. Hebu andika vyema herufi zifuatazo ili zionyeshe vyema majina hayo.

nuMug nyemwe vugun _____

Mrishau aw abuja _____

faMlme aw aamni _____

Baab aw leelim _____

KAZI YA KUFANYA

Hebu ifikirie ndoto ya Isaya alipokuwa hekaluni. Yafikirie yale ambayo Mungu alimwambia Isaya na jinsi alivyojibu. Sasa jifikirie wewe mwenyewe na yale ambayo Mungu anakutaka ufanye.

Hatua ya Kwanza: Ndoto au yale Isaya alijifunza kutoka kwa Mungu

Hatua ya Kwanza: (Andika hapa chini yale unayoelewa juu ya Mungu yu nani.):

Hatua ya Pili: Isaya alijiona jinsi alivyo mwenyewe.

Hatua ya Pili: Unaweza kujiona jinsi ulivyo wakati unapoelewa ukuu wa Mungu. (Andika hapa chini jinsi unavyojiona mwenyewe): _____

Hatua ya Tatu: Ombi la Isaya kwa Mungu na kusamehewa kwa dhambi zake

Hatua ya Tatu: (Andika katika nafasi ifuatayo yale uliyofanya juu ya dhambi iliyoko maishani mwako):

Hatua ya Nne: Isaya alielewa kwamba Mungu alikuwa akimwita mtu wa kunena ujumbe wake.

Hatua ya Nne: (Andika katika nafasi ifuatayo yale unayofikiri Mungu anataka kuwaambia watu wa siku hizi.): _____

Hatua ya Tano: Isaya aliitikia mwito wa Mungu.

Hatua ya Tano: (Eleza katika nafasi ifuatayo yale ambayo unatarajia kufanya kama mjumbe wa Mungu.): _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Kisha nikasikia sauti ya Bwana, akisema, Ninitume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, mimi hapa; nitume mimi” (Isaya 6:8).

Kuna watu wengi mahali unapoishi ambao hawajawahi kusikia ujumbe wa Yesu Kristo. Au pengine wamewahi kusikia tu, lakini hawajatii yale ambayo wamesikia. Unaweza kushiriki ujumbe wa Mungu kwa njia nyingi tofauti. Tumia muda fulani wiki hii kwa kufikiri juu ya yale ambayo Mungu anakutaka ufanye sasa. Fikiria pia yale ambayo anakutaka utekeleze maishani mwako.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA SITA

MIKA ANAELEZA MAHITAJI YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Mika 6:1-8

Tom na Petro walikuwa wame-simama nje ya kanisa. Walikuwa wamefika mapema ili wahudhurie darasa la Wakristo wapya. "Mchungaji Muturi ni mwalimu mzuri sana," Petro akasema. "Nimefurahi kwa sababu anatufundisha mengi kuhusu Mungu na yale anayotarajia kutoka kwetu kama Wakristo. Hapo zamani nilifikiri kwamba Mkristo alipaswa tu kuhudhuria kanisa na kutoa pesa kidogo."

"Je! Mungu hatosheki na hayo tu?" Tom akamwuliza. "Je! Hii si ndiyo maana ya kuwa Mkristo? Kwa kweli najua kwamba ni lazima ubatizwe. Kwani si hayo tu yanayo hitajika?"

Je! Ungejibuje maswali haya ya Tom?

Somo hili lihusulo nabii Mika litakusaidia kuelewa mahitaji ya Mungu kutoka kwa watu wake.

NABII MIKA

Mika alikuwa mkulima aliyeishi na kuhubiri kule Yuda. Nyumbani kwake

kulikuwa karibu na mji wa Morasuti karibu na mpaka wa Wafilisti. (Tafuta mji wa nyumbani kwa Mika kwenye ramani ulioko karibu kilomita 30 mashariki ya kusini mwa Yerusalemu. Mika alihubiri wakati wa siku za mwisho za huduma ya Isaya, mnamo mwaka wa 735-710 B.C. Isaya aliongea hasa juu ya wafalme, lakini ujumbe wa Mika ulikuwa wa kila mmoja. Ujumbe wake ulikuwa sawa na ule wa Amosi kwa sababu alisema mengi kuhusu udhuluma kati ya watu. Tofauti iliyoko ni kwamba Mika alitoa unabii wake akiwa kwao, Yuda. Hali Amosi aliishi Yuda naye akatoa unabii juu ya Israeli.

Je! Hali ilikuwaje nchini humo wakati huu wa Mika? Viongozi wa serikali na wale wa kidini wa Yerusalemu hawakumpendeza Mungu. Hawakujali mahitaji ya walio maskini. Lakini, waliwafikiria kwanza matajiri ambao wangewahonga. Viongozi hawa walijali sana utajiri kuliko kutenda yaliyomema. Mika aliwaambia watu juu ya dhambi hizi. Aliwaambia yale ambayo Mungu anataka.

ALIITWA KOTINI

Soma Mika 6:1-8. Pengine umewahi kusikia wazazi wako wakizungumzia jinsi tatizo linavyotatuliwa kule vijijini. Wazee wa kijiji hukutanika pamoja ili kusikiliza tatizo hilo. Hujadiliana juu ya tatizo hilo na mwishowe hufikia uamuzi fulani.

Watu walifuata desturi kama hii wakati ule wa Mika. Mtu ambaye alikuwa na malalamiko (mashtaka) fulani alienda uwajani kati ya lango la mji. Hatimaye, wazee waliitwa ili wasikilize lalamiko lake nao wakate shauri lihusuo tatizo hilo.

Tunajifunza kutoka kwa ujumbe huu wa Mika kwamba Mungu alikuwa na mashtaka. Yeye hakwenda katika lango la mji na kuwaita wazee wazungumzie, lakini alitumia mtindo huu kuwasaidia watu waelewe ujumbe wake.

Soma kifungu cha 1 na 2. Je! Mashtaka ya Mungu yalihusu nani? — . Ndiyo Mungu alikuwa na mashtaka juu ya Israeli. Neno hili “Israeli” linamaanisha watu wote wa Mungu, na si tu wale walioko katika Ufalme wa Kaskazini. Hasa Mika alikuwa akinena maneno ya Mungu kwa watu wa Yuda.

Milima na vilima vilikuwa mashahidi. Vyote viliitwa ili kusikiliza kisa hiki.

MASHTAKA

Soma tena Mika 6:3-5. Twamwona Mungu akitoa mashtaka juu ya watu hao. Mungu aliwauliza maswali mawili. Yote yanapatikana katika kifungu cha tatu. Yaandike katika nafasi ifuatayo:

Swali la Kwanza: _____

Swali la Pili: _____

Ndiyo, Mungu aliwauliza watu wake kwamba, “Enyi watu wangu, nimewatenda nini?” na “Je! Nani nimewachosa kwa habari gani?”

Hatimaye Mungu anaeleza jinsi alivyokuwa mwaminifu na mwema kwa watu wake. Anaendelea kusema jinsi alivyowatoa Waisraeli kutoka utumwani kule Misri. Alimzuia nabii Balaamu kwa kutowalaani watu wake walipopitia katika nchi ya Moabu. Aliwaongoza kwa usalama hadi katika Nchi ya Ahadi.

Sasa, baada ya miaka mingi kupita, watu wa Mungu walikuwa wamesahau jinsi Mungu alivyowasaidia.

JIBU LA WATU

Soma Mika 6:6-7. Watu walionekana kama hawajaelewa kabisa yale yaliyosemwa na Mungu. Walikuwa wamesahau maana ya ibada ya kweli. Ilionekana kama walidhania kwamba wangempendeza Mungu iwapo wangemtoa dhabihu fulani. Walikuwa wamesahau kwamba sadaka na dhabihu vilionyesha shukrani zao kwa baraka walizopata na kukiri kwa dhambi zao.

Je! sadaka na dhabihu zimeitwaje katika vifungu hivi?

1. _____ 2. _____
3. _____ 4. _____
5. _____

Sadaka ya mwisho iliyotajwa ilikuwa ile iliyotolewa na wale wasio Wakristo.

Mungu hakuwa anataka atolewe sadaka ya mtoto. Hii ingekuwa dhambi. Lakini, watu walifikiria kwamba pengine Mungu angependezwa na kutolewa kwa sadaka nyingi.

Ni rahisi kuona kwamba watu wa Mungu hawakuelewa kamwe maana ya kupenda na kumwabudu Mungu.

HUKUMU

Sasa ni wakati wa kusikiliza hukumu. Je! Jibu litakuaje? Je! Mungu anawataka watu wake wafanyeje?

Mungu amewaonyesha watu wake yale yanayohitajika. Aliwatajia mambo matatu ambayo wanapaswa kufanya. Hebu andika vizuri herufi zifuatazo ili zieleze maneno hayo.

TEAND KHIA _____

PANUKDE MEHARE _____

NDAKWE KAW VUNYEKEUNYE
AN NUMUG WOKA _____

Mungu angali anahitaji mambo haya hata sasa. Anataka nasi tuyatende. Je! Unaelewa jinsi ya kutekeleza mahitaji haya?

“Kutenda haki” inamaanisha kufanya yaliyomema na mazuri. Wafuasi wa Mungu hawapaswi kudanganyana, wala kupokea hongo. Wanapaswa kuwasaidia maskini. Unapowatendea wenzako wema kuwa unaonyesha kwamba unataka kumpendeza na kumtukiza Mungu.

“Kupenda rehema” inamaanisha kwamba utawajali wenzako. Utaonyesha kujali kwako kwa matendo yako.

“Kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako” inamaanisha jinsi unavyomfikiria na kumtendea Mungu. Utagundua kwamba Mungu

anakupenda naye ni mwaminifu. Utaelewa kwamba wewe ni mwenye dhambi na mdhaifu, lakini Mungu anaweza kukupa nguvu. Utataka kuishi maisha yanayompendeza Mungu.

KAZI YA KUFANYA

Soma tena Mika 6:3-5. Mungu, katika vifungu hivi ametaja baadhi ya mambo yaliyotokea katika maisha ya Israeli ambayo yalionyesha wema na uaminifu wake kwao.

Hapa chini kuna orodha ya mambo ambayo Mungu aliwafanyia Waisraeli: Andika namba katika kila nafasi iliyoachwa ili kufuatanisha jinsi yalivyotendeka, kuanzia tendo la kwanza hadi la mwisho. Namba ya kwanza, yaani 1, imeshaandikwa katika nafasi ifaayo.

— Daudi alimwua Goliati katika vita.

— Yusufu anaikoa jamaa yake isiangukie kwa sababu ya njaa.

— Mungu anawapa Waisraeli chakula cha mana kutoka mbinguni.

— Kuta za Yeriko zinabomoka mbele ya jeshi la Israeli.

— Mungu aliwapelekea Wamisri misiba kumi.

— Bahari ya chumvi iligawanyika.

— Sulemani ajenga Hekalu kule Yerusalemu.

— Mungu anawapatia Waisraeli nyama ya kula wakiwa jangwani.

— Mungu anazungumza na Musa katika kijiti kiwakacho moto.

1 Mungu anafanya agano na Ibrahimu.

Hebu irudie tena ili orodha ya miaka iliyoko katika somo la kwanza. Isome ili ufahamu muda ambao kila nabii alihubiri. Pengine hutaweza kukumbuka miaka hii yote, lakini jaribu kukumbuka jinsi manabii hawa walivyofuatana na kuhubiri.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"...na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!" (Mika 6:8).

Kifungu cha kukumbuka kina-kuambia mambo matatu ambayo Mungu anakutaka ufanye. Jambo la tatu ni "kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako". Hili linaonekana kama ni wazo zuri. Je! Linamaanisha nini?

Mungu alitembea pamoja na Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni. Hii inaonyesha kwamba walishiriki pamoja. Hata ingawa Mungu ni mkuu na mtakatifu, anataka awe na ushirika nasi. Anataka kwenda pamoja nasi.

Je! Tunaendaje pamoja na Mungu? Hatua ya kwanza ni kuukubali mpango wake wa wokovu. Kila mmoja ametenda dhambi. Kila mmoja amejaribu kuenenda katika njia yake mwenyewe. Kuna njia moja tu ambayo unaweza kuanzia kwa kumfuata Mungu. Nayo ni kutubu dhambi zako na kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako.

Hatua ya pili kuwa na wakati wa pekee pamoja na Mungu kila siku. Unaweza pia kumsikiliza akizungumza nawe kupitia kwa Roho Mtakatifu wakati unapoomba. Mungu huongea nawe pia kupitia kwa Neno lake ambalo ni Biblia. Je! Unahitaji kusaidiwa katika mwenendo wako wa kila siku?

Mwombe mwalimu wako orodha ya mpango wa kukuwezesha kusoma Biblia yote. Mwulize kuhusu kitabu kiitwacho, *Nifuate*. Tumia masomo yako ya Biblia kila siku ili yakusaidie kwa kusoma na kuielewa Biblia.

Hatua ya tatu ni utiifu. Si rahisi kuwa mtiifu. Lakini Mungu atakupa nguvu za kukuwezesha kuishi jinsi inavyotakikana. Unapaswa tu kumwomba nguvu hizi.

Hebu zifikirie hatua hizi tatu na uandike katika nafasi iliyoachwa hapo chini yale ambayo unatarajia kufanya kwa kila mojawapo.

Hatua ya Kwanza: _____

Hatua ya Pili: _____

Hatua ya Tatu: _____



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA SABA
NENO LA BWANA LAMJIA SEFANIA

MASOMO YA BIBLIA: Sefania 1:1-6,
12; 3:17-20

Je! Wewe hufurahia kusikiliza redio au television inapotangaza habari? Kila siku kuna habari nzuri na habari mbaya. Yule anayesoma habari anaweza kutangaza juu ya hospitali mpya ambayo inaenda kufunguliwa



rasmi na raisi katika sehemu ya mashambani. Hii ni habari nzuri. Msomaji yule yule anaweza pia kutangaza habari za watu walio na njaa kule sababu mvua haijanyesha katika eneo lao. Hii ni habari ya kuhuzunisha.

Nabii aitwaye Sefania, alikuwa na habari njema na habari ya kuhuzunisha kwa watu wa Yuda. Habari za kuhuzunisha ilikuwa kwamba hukumu ya Mungu ingetolewa kwa kila mmoja. Yuda ilikuwa na hatia ya kuabudu sanamu na kuthamini sana utajiri. Siku ya Bwana ilikuwa inakaribia, wakati ambapo Mungu ataadhibu kutotii kwake.

Habari njema ilikuwa kwamba kulikuwa na tumaini kwa sababu Mungu angewafanya upya watu wake. Mwishowe, kungekuwa na furaha nao watu wangepata baraka za Mungu baada ya siku ya Bwana.

SEFANIA

Sefania alitoa unabii wakati Yosia alipokuwa mfalme wa Yuda. Sefania

alikuwa na ukoo mmoja na mfalme. Alizaliwa katika jamaa wa cheo na akanena na uwezo mkuu.

Kulikuwepo na watawala waovu sana kabla ya Yosia kuwa mfalme. Manase, babu yake Yosia, alikuwa mmojawapo wa wale wafalme waovu. Alitawala Yuda kwa muda wa miaka arobaini na mitano na akaliongoza taifa hilo katika kutoabudu Mungu wa kweli. Aliendeleza uabuduiji wa sanamu, akajenga madhabahu ya kumwabudia Baali na akasisitiza uabuduiji wa nyota.

Yosia alianza kutawala alipokuwa na umri wa miaka minane. Alianza kuleta mabadiliko nchini humo alipofikia umri wa miaka ishirini. Neno la Mungu, yaani Amri ya Musa, lilikuwa limepoteza kwa miaka mingi sana. Yosia alisisitiza ufundishaji wake wakati zilipopatikana. Ni katika wakati huu ambapo Sefania alianza kazi yake. Pengine Sefania alimdokezea Yosia juu ya mabadiliko haya aliyoyafanya.

Jina la Sefania linamaanisha kwamba, "Yule ambaye Mungu amemficha au amemlinda." Pengine wazazi wa Sefania walikuwa wakimpenda Mungu na iliwabidi wamfiche mwanao ili awe salama.

UJUMBE WA SEFANIA

Kiini cha ujumbe wa nabii huyu ni hukumu juu ya dhambi. Taifa hili lilikuwa limepoteza ufahamu wake wa mema na mabaya. Hawakuonea haya matendo yao, naye Mungu alikuwa tayari kuwaadhibu.

Sefania aliwaonya kwamba siku ya Bwana, ambayo ni siku ya hukumu ya Mungu kwa watu wa Yuda, ilikuwa

imekaribia. Watu wa Yuda walikuwa wameanza kufikiria na kutenda kama jirani zao waovu, yaani, Waashuru. Kulikuwa na uabuduiji wa Baali (1:4), uabuduiji wa nyota (1:5), uvaaji wa mavazi ya kigeni (1:8), udhalimu na udanganyifu (1:9), na zaidi ya yote hawakujali juu ya dhambi zao. Walisema kwamba, "Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya" (1:12b).

Mwardishi anaonekana kama alikuwa amekasirika sana alipoanza ujumbe wake. Aliwaonya kwamba mkono ule ule ambao uliwaokoa kutoka utumwani kule Misri ndio ambao ungewaadhibu. Siku ingekuwa ya shida, taabu, mawingu na giza kuu. Yote haya yangetokea kwa sababu walikuwa wamemtendea Bwana dhambi. Sefania alitoa pia unabii juu ya mataifa yaliyo jirani ya Yuda. Gaza na Wafilisti walioko upande wa magharibi wataangamizwa. Moabu ambao wako upande wa mashariki watakuwa kama Sodomu. Amoni nao watakuwa kama Gomora. Waithiopia (wa Kushi) ambao wako upande wa kusini watauawa kwa upanga. Ninawi, ambayo ni mji mkuu wa Ashuru iliyoko kaskazini, itaangamizwa kabisa.

Mwishowe Sefania alitoa unabii juu ya Yerusalemu, mji wa Mungu. Watu walikuwa waovu na viongozi wao walikuwa kama simba wangurumao. Manabii na makuhani walitumia vyeo vyao kwa manufaa ya kibinafsi badala ya kuwaonya watu juu ya mahitaji ya Mungu. Sefania aliwaomba watu watambue kwamba hukumu ya Mungu inakaribia nao watubu wakati huu wanapoweza.

Sefania alimalizia ujumbe wake na maneno ya tumaini. Kulikuwepo na wale ambao wangebakia waaminifu kwa Bwana. Mungu angekuwa pamoja nao na angewasaidia. Wao wangesamehewa dhambi zao na wangemwabudu Bwana kwa furaha.

FUNDISHO LA UJUMBE HUU WA NABII KWETU

Watu wa Yuda hawakujali mafundisho ya Mungu. Walidhania kwamba Mungu hakujali kamwe. Waliacha maovu ya majirani zao waovu, Waashuru, kuwa ndiyo mwongozo wa maisha yao. Waliacha wadhuriwe na Waashuru, badala ya wao kuwasaidia Waashuru kujua Mungu wa kweli.

Siku hizi kuna kudhuriwa kuzuri na kubaya. Unapaswa kujiuliza iwapo unayaacha maovu yatawale tabia zako. Jiulize mwenyewe iwapo mambo yafuatayo yanakusaidia kumfahamu Mungu vyema au ikiwa yanakuhimiza kufikiria maovu. Weka alama ya (✓) kwenye mambo yaliyo mema kwako na alama ya (x) kwenye mambo yanayokueleza kutenda maovu maishani mwako.

_____rafiki zako

_____vitabu usomavyo

_____sinema uonazo

_____vipindi vya televisioni unavyoona

_____nyimbo unazoimba sana

KAZI YA KUFANYA

Siku hizi tuna Neno la Mungu. Ni kitabu cha mwongozo ambacho kinatusaidia kujua jinsi ya kuishi. Jibu maswali yafuatayo yanayohusu Neno la Mungu maishani mwako. Jibu kwa kusema Ndiyo au La.

_____Ninasoma Neno la Mungu kila siku.

_____Kila siku nasikiliza mahubiri ya Neno la Mungu.

_____Kila wiki najaribu kukariri kifungu kimoja kipya.

_____Ninajifunza Neno la Mungu kwa muda wa nusu saa kila wiki.

_____Kila wiki huwa natafakari juu ya kifungu kimoja cha Biblia.

Yaache yale uliyojibu La ya kuonyeshe jinsi unavyotaka kulifanya Neno la Mungu liwe la muhimu maishani mwako. Sefania aliwaambia watu watubu kwa sababu "Siku ya Bwana ilikuwa karibu." Soma vifungu vifuatavyo vya sura ya 1 na uandike usemi ambao unaeleza siku hii ya hukumu ya Mungu.

Kifungu cha 4: _____

Kifungu cha 7: _____

Kifungu cha 14: _____

Kifungu cha 15: _____

Kifungu cha 15: _____

Kifungu cha 15: _____

Andika neno KOSA au SAWA kando ya kila mojawapo ya usemi ufuatao:

- a. ____ Hukumu ya Mungu iliwahusu tu wale walioishi katika mataifa ya kigeni. (1:2-3)
- b. ____ Siku ya hukumu ya Mungu kwa watu wake ilikuwa inakaribia. (1:6-7)
- c. ____ Yerusalemu hainge-hukumiwa. (1:4)
- d. ____ Baadhi yao walisema kwamba, "Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya." (1:12)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Wala msifuatisha namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:2).

"Kufuatisha" kunamaanisha kuiga hali na maelekezo na desturi za wengine. Taja njia moja ambayo unauacha ulimwengu udhihirishe tabia na mazoea yako.

"Kugeuzwa" inamaanisha ku-badilisha tabia na mwenendo. Mungu anakutaka utende na ufanane na Yesu. Hebu fikiria jambo ambalo utafanya wiki hii ambalo litakufanya ufanane na Yesu. Liandike katika nafasi ifuatayo na umwombe Mungu ili akusaidie uwe mwaminifu kwa kulifanya.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA NANE

NAHUMU NABII WA MAANGAMIZI

MASOMO YA BIBLIA: Nahumu
1:1-3, 12-14, na 3:5-7

Mvua ilikuwa imeanza kunyesha katika nchi moja ya Kusini mwa Afrika na ukawa ni wakati wa kupanda mbegu za mahindi. Kefa alitembea shambani mwake na watoto wake wawili Tom na Bob. Baba yao alikuwa amewafundisha vijana hawa kazi ya shamba tangu walipokuwa wadogo. Mwaka huu Tom na Bob walitakiwa kupanda mimea hiyo bila kusaidiwa na baba yao.

Tom na Bob walianza kazi ya kupanda mara tu jua lilipoanza kuchoma juu ya vilima vilivyokuwa nyuma ya nyumba yao. Walifanya kazi asubuhi yote bila kupumzika. Mara tu baada ya chakula cha mchana na kupumzika kidogo, walirejea tena kwa kazi yao.

Ilipofika jioni, vijana hawa walikuwa wamechoka sana, na hali kulikuwa bado kuna mbegu nyingi za kupanda. Bob akafikiria jambo la kufanya. Wangemaliza pale walipokuwa wakipanda halafu wachimbe shimo ili wazifunike humo zile mbegu zilizobakia. Tom alikubali naye.

Yote yaliendelea vizuri hadi wakati ambapo mbegu zilianza kumea. Kefa aliamua kutembea shambani ili ajionee vile mimea mipya inavyokua. Alipofika mwisho wa msitari aliona mimea mingi ikiwa imemea kutoka mahali pamoja. Alitambua mara moja kile kilichofanyika. Aliwaita Tom na Bob ili kujua sababu ya haya yote. Walimweleza baba yao yote waliyoyatenda.



Tom akasema, “Nilidhani kwamba hungejua vile tulivyozifanyia mbegu hizo hizo.” Baba yao mwenye hekima akawaambia, “Wanangu, hili liwe fundisho kwenu. Kumbukeni kwamba itajulikana wazi mnapofanya kosa lolote. Biblia inasema kwamba, “..nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yetu itawapata hapana budi.” (Hesabu 32:23b)

Ujumbe wa nabii Nahumu unafanana na onyo la Kefa alilowapatia wanawe. Nahumu alitoa unabii kwamba Ninawi, mji mkuu wa Ashuru, utaangamizwa kabisa. Mji huo na taifa lote kwa jumla walikuwa wametenda dhambi kwa muda wa miaka mingi mbele za Bwana. Walikuwa wakifanya hivyo kwa sababu ya uwezo na nguvu zao nyingi ikilinganishwa na mataifa mengine. Kwa hivyo Ninawi ingeadhibiwa kwa sababu ya dhambi zake, na hakuna yule ambaye angeweza kuiokoa.



NAHUMU

Nahumu alikuwa nabii wa Mungu wakati wa Sefania na Habakuki. Mungu alimwonyesha katika maono wakati ambapo Ashuru ingeadhibiwa kwa makosa yake. Nahumu aliongea waziwazi kwa mji mkuu wa Ninawi ambao uliwakilisha taifa lote.

Nahumu alikuwa mwenyeji Yuda aliyetoka katika mji wa Elkoshi. (1:1) Ni machache tu yanayojulikana maishani mwake isipokuwa kwa unabii wake. Jina lake linamaanisha “mfariji”. Kunao uhakikisho kwa Yuda hata ingawa ujumbe wa ufariji haujahimizwa sana katika kitabu chake. Wale ambao walikuwa wakiwafanya watu wa Mungu wataabike wangeangamizwa. Mtu mmoja alisema kwamba, “Nahumu hakujua cho chote, lakini alifanywa mtu mashuhuri katika mikono ya Mungu.” Mungu alitumia ushairi wake kuonya Ninawi na kuleta ufariji katika Yuda.

UJUMBE WA NAHUMU

Mji wa Ninawi ulikuwa mkuu sana ulimwenguni wakati wa unabii wa Nahumu. Ulikuwa mkubwa, wenye utajiri na uliojaa maovu. Nahumu alikataza dhambi zake za wizi, uabuduji sanamu na uchawi. Mji huu ulikuwa ukitumia nguvu za kijeshi kuyaangamiza mataifa mengine madogo. Wafanye biashara wake walikuwa wakiwatumia wengine ili wajitajirishe wao wenyewe.

Yona alikuwa amekwisha kwenda huko na kuhubiri ujumbe wa kutubu miaka mingi kabla ya Nahumu. (Yona 3:5) Watu walimsikiliza na kuyafuata maneno yake lakini hawakubakia waaminifu kwa Mungu. Nahumu

aliuona mji huo kama, "Mji wa damu! umejaa mambo ya uongo na unyang'anyi." (Nahumu 3:1) Unabii wake ulikuwa juu ya Ninawi, lakini ulitoa uhakikisho kwa wale waliobakia waaminifu kwa Mungu.

Ujumbe wa Nahumu ulianza kwa kueleza utukufu wa Mungu. Yeye ni Mungu wa wivu, bali pia ni Mungu wa kweli. Haonyeshi haraka hasira yake juu ya dhambi. Mungu si mwepesi kukasirika, lakini hawezi kuacha kuadhibu dhambi.

Nahumu alianza kuwafariji watu wa Yuda katika sura ya 1:12-14. Ingawa taifa la Ashuru, lililowakilishwa na mji wake mkuu, Ninawi, lilionekana lenye nguvu nyingi, lingeisha. Wakati ungefika ambapo hata jina lake halingekumbukwa kamwe.

Nahumu 3:5-7 inaeleza hasira ya Mungu kwa Ninawi. Mji huu ungetendewa kama mwanamke mwovu, malaya, aliyeisaliti nchi yake. Utadharauliwa kabisa.

Historia inaonyesha kwamba Ninawi iliangamizwa kama vile nabii alivyoeleza. Mnamo mwaka wa 612 B.C., Wakaldayo na Wamede waliuvamia na wakauteketeza kwa moto mji huo wote. Mataifa jirani yalifurahia kuangamizwa huko. Mahali ambapo mji wa Ninawi ulikuwa, hapangeweza kupatikana baada ya miaka mamia kupita. Hii inatufundisha kwamba hakuna taifa au mji, hata uwe na nguvu nyingi ambao utaepuka hukumu ya Mungu.

FUNDISHO LA UJUMBE WA NABII HUYU KWETU

Watu hawasemi mengi kuhusu dhambi. Hatupendi kukubali kwamba

tumekosa wala kutenda mabaya. Paulo, katika Warumi 3:23 anatuambia kwamba, "...wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

Mungu habadiliki. Hakuidhinisha dhambi za Ninawi na vivyo hivyo haidhinishi dhambi zetu. Mji wetu, taifa letu, na hata sisi wenyewe tutahukumiwa na Mungu. Inaweza kuonekana kwa muda mchache kwamba kila kitu kiko shwari. Lakini Mungu ni mvumilivu. Hupatia taifa na watu kwa jumla nafasi za kutubu. Alimtuma Yona kuonya Ninawi. Anamruhusu kila mmoja wetu kusikia ukweli kuhusu dhambi na adhabu yake, na kuhusu upendo na wokovu wake. Sisi ndio huchagua matokeo. Tunaweza kupata msamaha kupitia kwa Kristo Yesu. Au, tutaipitia ghadhabu ya Mungu wakati wa hukumu.

KAZI YA KUFANYA

Soma Nahumu 1:1-3 na uandike jinsi Mungu atakavyoitendea dhambi.

Kifungu cha 2: "Bwana ni Mungu mwenye wivu, naye hujilipizia k _____

Kifungu cha 2: "Bwana hujilipizia k _____ juu ya adui zake."

Kifungu cha 3: "Bwana si m _____ wa h _____, ana uweza mwingi."

Kifungu cha 3: "...wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana h _____ kamwe."

Nahumu 1:12-14 ina ujumbe na maonyo juu ya Ninawi na ujumbe wa kufariji juu ya Yuda. Andika herufi N kando ya usemi unaoeleza juu ya Ninawi na herufi Y kando ya usemi unaoeleza juu ya Yuda.

Kifungu cha 12: _____ “Ijapokuwa wana nguvu zilizo timilifu, ijapokuwa ni wengi, hata hivyo watakatwa, naye atapita na kwenda zake.”

Kifungu cha 12: _____ “Ingawa nimekutesa, sitakutesa tena.”

Kifungu cha 13: _____ “Na sasa nitakuvunjia nira yake, nami nitakupasulia mafungo yako.”

Kifungu cha 14: _____ “Bwana ametoa amri katika habari zako, ya kwamba asipandwe tena mtu awaye yote mwenye jina lako.”

Kifungu cha 14: _____ “Nitakufanyia kaburi lako; kwa maana u mbovu.”

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Bwana ni mwema, ni ngome siku ya taabu, naye huwajua hao wamkimbiliao” (Nahumu 1:7).

Kifungu chetu cha kukumbuka kinatambua mambo matatu yahusuyo Mungu.

1. Yeye ni mwema.
2. Yeye ni ngome.
3. Yeye huwajua hao wamkimbiliao.

Andika katika nafasi ifuatayo sababu iufanyao ujumbe huu kuwa wa muhimu kwa watu wa Yuda.

MUNGU NI MWEMA. Taja njia moja ambayo Mungu ni mwema kwako.

NI NGOME SIKU YA TAABU. Neno hili “Ngome” linamaanisha mahali pa usalama. Ni kama boma lililojengwa kwa ajili ya usalama. Je! katika njia gani unahitaji Mungu awe ngome ya maisha yako? _____

NAYE HUWAJUA HAO WAMKIMBILIAO. Hii inatukumbusha kwamba Mungu anatumbea. Anatualika tumwendee ili atusaidie. Kumkimbilia kunamaanisha kutafuta “makao au ulinzi wakati wa hatari.” Je! Unahitaji kumkimbilia Mungu wakati wa shida, matatizo au hatari? Andika sala lako kwa Mungu na umwombe awe kimbilio lako wakati wote. _____



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved


SURA YA TISA
HABAKUKI, NABII WA MASWALI

MASOMO YA BIBLIA: Habakuki
1:1-4, 12-13; 2:2-4; 3:17-19

Je! Umewahi kuuliza swali hili, "kwa nini ni mimi tu?" Pengine umesoma kwa bidii ili ufanye mihani lakini mwishowe

unakosa kufaulu vizuri. Hali kunaye mwingine ambaye hasomi kamwe, lakini anafaulu vizuri. Mwishowe unajiuliza, "kwa nini ninapatwa na mabaya ninapojaribu kutenda mema na

Dunia ya Manabii



hali hakuna lifanyikalo libaya kwa wale ambao hawajaribu lo lote?"

Habakuki, ambaye alikuwa nabii wa Yuda aliyeishi wakati wa utawala wa Mfalme Yehoiakimu, aliuliza swali kama hili kuhusu watu wake. Akamwuliza Mungu, "Mungu, mbona ni sisi tu?"

Habakuki aliona ukatili na uovu uliokuwa ukifanywa. Watu wa Mungu walikuwa wakiteseka kwa sababu ya wale waovu na Habakuki alishangaa ni kwa nini iwe hivyo. Wakaldayo (waliotoka Babeli) walikuwa wameteka mataifa madogo madogo nao walikuwa wakiyaangamiza. Na sasa walikuwa wanatisha kuivamia Yuda ambayo ni nchi yake. Habakuki akamwuliza Mungu, "Je! Unataka uliruhusu taifa hili ovu lituangamize, sisi wateule wako?"

Kama Habakuki angekuwa akiishi sasa nao waandishi wa habari waende kumhoji, basi habari yake ingekuwa kama hii:

GAZETI LA MATAIFA YA BIBLIA YUDA 606 B.C.

Nabii Habakuki amesikilizwa sana kwa muda mrefu na watu wa taifa la Yuda. Imeonekana kwamba amekuwa akiongea na Bwana juu ya shida zetu. Hali katika nchi yetu ya Yuda ni nzuri sana. Israeli ambapo ni taifa lililo ndugu yetu upande wa kaskazini, liliangamizwa na Waashuru karibu karne moja iliyopita. Nao Waashuru wakaangamizwa na Wababeli. Na sasa sisi tunatishwa na Wababeli.

Tulianza kupata shida miaka michache iliyopita baada ya kifo cha Mfalme Yosia. Alikuwa mfalme mwema na alileta mabadiliko mengi

yaliyohitajika nchini kwetu. Sasa mabadiliko yote aliyoanzisha yanaanza kutoweka taratibu. Hali ya maisha katika Yuda imekuwa mbaya sana kuliko hapo awali.

Juzi nilienda hekaluni ili kumtembelea nabii Habakuki. Nayo mazungumzo yetu yakawa kama ifuatavyo:

Mwandishi: Nabii Habakuki, Je! Ni kweli kwamba ulilalamikia Mungu watu wa Yuda wanavyotendewa?

Habakuki: Ndiyo, ni kweli kwamba nilimwendea Mungu nikiwa na maswali kadhaa yahasuyo jinsi hali ilivyo nchini kwetu.

Mwandishi: Je! Ulilalamikia nini?

Habakuki: Nilimwuliza Mungu kwamba wale walio waaminifu watateseka kwa muda gani hali wale walio waovu wanazidi kuendelea? Kuna maovu mengi yanayoendelea nchini. Matajiri na maskini wanashiriki katika kuvunja sheria, lakini hawaadhibiwi.

Mwandishi: Je! Mungu amejibu swali lako?

Habakuki: Ndiyo, jibu limekuja. Mungu anatutaka tuwe macho na tuone yale atakayofanya. Anajua wakati mzuri wa kuwaadhibu waovu, nasi tunapaswa kuvumilia.

Mwandishi: Je! Ni swali gani tena ulilomwuliza Mungu?

Habakuki: Swali langu lilikuwa hivi, kwa nini Mungu anawatumia wale waovu kwa kuwaadhibu wale ambao si waovu sana?

Mwandishi: Je! Unaweza kueleza kwa kifupi yale unayomaanisha kwa swali hili?

Habakuki: Najua ukatili na uovu wa Yuda. Tumekuwa watu wasiotii na kwa hivyo tunapaswa kuadhibiwa. Je! Mungu ataiacha Yuda iliokuwa ovu kuadhibiwa na taifa ambalo ni ovu zaidi kuliko Yuda?

Mwandishi: Je! Mungu alijibuje swali lako hili la pili?

Habakuki: Wale waovu, ambao ni Wakaldayo waliotoka Babeli, wataadhibiwa, lakini walio wa haki na wema wataishi kwa imani.

Mwandishi: Nimesikia kwamba walio wa haki na wema wataishi kwa imani, lakini, je! jambo hili litawezekanaje hali Mungu amenyamaza tu?

Habakuki: Ni lazima mtu aliye na ushiri mwema na Mungu aishi kwa imani kwa kutojali yale yanayofanyika pale alipo. Anajua kwamba Mungu ndiye mtawala, naye humwamini hata ingawa haielewi jambo hilo.

Mwandishi: Je! Unadhani watu wataitikiaje jibu hili la Mungu?

Habakuki: Ni rahisi kumtumikia Mungu wakati mambo yanapokwenda vizuri. Watu huanza kumlaumu Mungu wakati wapatwapo na shida. Hawaelewi kwamba shida zao hata hutokea kwa sababu ya uovu na matendo yao.

Mwandishi: Je! Mungu alikwambia wakati ambapo adui zetu wataadhibiwa?

Habakuki: La, hakuniambia, bali alisema tu kwamba kutatokea hivyo. Ataleta hukumu wakati atakaopenda mwenyewe.

Mwandishi: Je! Utawaambia watu ujumbe ambao umepewa na Mungu?

Habakuki: Nitawaambia. Hata Mungu mwenyewe aliniambia niuandike vizuri ili wote waweze kuusoma.

Mwandishi: Hebu tuambie sasa yale unayofikiria juu ya Mungu.

Habakuki: Mungu ni mwenye haki. Mimi mwenyewe namwita "Mtakatifu." Huelewa shida zetu naye hututunza. Hata hashangai kujua kwamba tunateswa na walio waovu.

Ametupa miguu kama ya kulungu (aina ya mnyama anayepatikana jangwani.) Wao huishi katika sehemu mbali mbali hali hawajikwai wala kuanguka. Miguu yao huwafanya wawe salama hata wapandapo juu milima au miamba. Mungu ndiye nguvu zetu, yeye atatulinda hata wakati wa hatari.

Mwandishi: Asante sana Nabii Habakuki. Kutokana na maoni yako nimeona kwamba watu wa Yuda wana mambo mawili ya kuchagua. Tunaweza kumsahau Mungu na kuishi bila tumaini. Au, tunaweza kumwamini Mungu na kuamini kwamba anajua majibu yote.

Fundisho la Ujumbe wa Nabii Huyu Kwetu

Wewe nawe una uchaguo huu wa kufanya anapoona mabaya yaki-tendeka kwako tu wala si kwa wenzako. Au, unaweza kujitoa kwa Mungu na umwamini kwamba utaondoa shida zako katika wakati wake mwenyewe. Hebu fikiria juu ya Habakui 3:19. Je! Inamaana gani kwako kwamba Mungu huifanya miguu yetu kuwa kama ya Kulungu? Jambo hili linapaswa kukukumbusha juu ya agizo la Mungu la kukupa nguvu, kukulinda

na kukupa uwezo wa kuvumilia wakati wa shida.

KAZI YA KUFANYA

A. Soma Habakuki 1:1-4. Andika swali ambalo Habakuki aliuliza kwanza katika maneno yako mwenyewe.

Swali la kwanza: _____

Soma Habakuki 1:13, na uandike lile swali la pili ambalo Habakuki aliuliza.

Swali la pili: _____

Sasa andika swali ambalo ungependa kuuliza. _____

B. Soma Habakuki 2:2-4, na uweke alama hii (✓) kando ya jibu lililo sahihi.

1. Jibu la Mungu kwa Habakuki lilikuwa:

(a) Liwe kama siri

(b) Liandikwe vizuri juu ya mbao za mawe.

(c) Lisomewe makuhani kule hekaluni.

2. Mungu alisema kwamba jibu lake lingekuwaje:

(a) Halingevunjwa.

(b) Lingetimia.

(c) Lingechelewa kwa muda mrefu.

3. - Mungu alisema kwamba watu wanapaswa waitikie kwa:

(a) kuishi kwa imani.

(b) kuwaambia viongozi juu ya shida zao.

(c) kujihurumia wenyewe.

C. Soma Habakuki 3:18-19. Nabii huyu aliitikia mwito wa Mungu kwa kuomba. Andika katika nafasi ifuatayo jinsi Mungu alivyo kwa Habakuki.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Tazama, roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake, lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake” (Habakuki 2:4).

Andika maelezo mafupi ya maneno haya matatu yaliyo ya muhimu katika kifungu hiki.

Haki _____

Kuishi _____

Imani _____



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA KUMI
MPANGO WA MUNGU KWA YEREMIA

MASOMO YA BIBLIA: Yeremia
1:6-9; 18:1-6

Yeremia, kama manabii wengine tuliojifunza habari zao, alikuwa akitoka katika nchi ya Yuda. Alinena kwa niaba ya Mungu wakati wa shida sana kulingana na historia ya taifa hili. Aliendelea kuwahimiza watu wawe waaminifu kwa Mungu hata ingawa aliteswa sana kwa kusema ujumbe wa Mungu.

Hebu jifikirie kwa muda mfupi kwamba wewe ni Yeremia, na kwamba hadithi hii inahusu wewe.

Baba yako ni kuhani, kwa hivyo unaendelea kukua huku ukisikia habari za Mungu. Watu wote waliokaribu nawe wanaabudu sanamu. Wao wanaiba, wanadanganya na kusema uongo karibu na hekalu. Nawe unashangaa kwa nini Mungu hawaadhibu.

Unajua kwamba Israeli, taifa ambalo lilikuwa kaskazini mwa Yuda liliangamizwa kwa sababu watu wake

walikosa kumtii Mungu. Hatimaye unajiuliza, "Je! Hakuna mtu ye yote hapa ambaye atawakanya watu? Kwa kweli Mungu yuko tayari kutoa hukumu yake kwetu."

Baadaye unamsikia Mungu akisema, "Yeremia nataka useme kwa niaba yangu." Jambo hili linakushangaza sana kwa sababu wewe ungali mtoto. Mungu anakwambia kwamba alikuwa na mpango nawe wa kuwa nabii hata kabla ya kuzaliwa.

Nawe unamwambia Mungu, "Bwana, mimi siwezi kusema. Hata hivyo ningali tu mtoto na huenda watu wasinisikilize kamwe." Naye Mungu anakukemea, kwa kukwambia, "Usiseme kwamba, 'mimi ni mtoto'; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru." (Yeremia 1:7) Mwishowe Mungu anakwambia kwamba usiogope kwa sababu atakuwa pamoja nawe.

Maneno ambayo Mungu anakwambia useme niyakuhunisha sana.

Nchi yako iko karibu kuvamiwa na Wakaldayo waishio katika Ufalme wa Kaskazini. Watu hawaamini unapowaambia ujumbe wa Mungu. Wao wanakwambia kwamba, "Wacha kutuambia habari hii ya kuhuzunisha. Hatutaki kuisikia kamwe. Yale yaliyoipata Israeli hayawezi kufanyika kwetu. Huu ni mji wa Daudi. Hata Hekalu liko hapa. Mungu hawezi kuacha kitendo kile kile kilifanya Yerusalemu.


Mwishowe unaamua kuacha, lakini Mungu anazidi kukwambia uendeleo kuwaambia ujumbe wake. Hatimaye unasikia habari za kusisimua. Sehemu ya sheria za Mungu imepatikana na ambao walikuwa wakilijenga upya Hekalu. Mfalme Yosia anasema kwamba sheria hizi zisomwe mbele ya watu wote. Halafu anawaamuru waharibu na kuondoa sanamu zote na wamwabudu Mungu pekee.

Nawe unafurahi kwa sababu unafikiria kwamba Mungu atabadili. Hatimaye, jambo lingine la kuhuzunisha linatokea kwa ghafula. Mfalme anafariki nao watu wanausahau ujumbe wa Mungu. Wanaanza tena kuabudu sanamu. Unaendelea tu kuwaonya lakini wao wanazidi kukwambia tu, "una kichaa."

Siku moja Mungu anakutuma nyumbani kwa mfinyanzi. Nawe unamwangalia akichukua udongo na kuanza kuufinyanga. Anailowesha mikono yake na kuanza kuufinyanga udongo ule juu ya gurudumu liliko mbele yake. Wakati mfinyanzi hapendezwi na chungu alichotengeneza, huharibu tena udongo ule na kuanza upya. Mungu anakufundisha jambo fulani wakati ulipo nyumbani kwa mfinyanzi huyu.

Jambo ambalo Mungu anakutaka ujifunze ni kwamba sisi ni kama udongo. Naye Mungu ni mfinyanzi. Atatuvunjavunja iwapo tutakataa kufuata mpango wake kwetu. Baadaye ataanza kututengeneza tena tuwe kitu cha maana. Yeye anatumbeza na hataacha kufanya kazi pamoja nasi.

Jeshi la maadui lilikuja Yerusalemu na likachukua baadhi ya watu wako na kuwapeleka Babeli jinsi Mungu alivyokwambia. Manabii wa uongo wanaanza kusema kwamba wale waliotekwa watarudi kwao. Wewe mwenyewe unajua kwamba hii si kweli kwa hivyo unawaandikia wale watu waliotekwa barua. Hii ndiyo barua uliyoandika.



Umekuwa ukihubiri kwa muda wa miaka ishirini wakati Mungu anapokwambia sasa uandike ujumbe wake katika kitabu. Rafiki yako Baruku anakusaidia kuandika. Yeye anaandika maneno yale unayomwambia. Baada ya kumaliza kuandika anapeleka kitabu hicho Hekaluni na kukisoma mbele ya watu.

Mfalme Yehoiakimu anasikia habari ya kitabu hicho na anawatuma watu kuja kukichukua. Nawe unadhania kwamba atayasikiliza maneno ya Mungu. Lakini, mfalme anachukua kitabu hicho na kukikatakata na kukichoma kwa moto. Kitendo hiki kinakukatisha tamaa, lakini huachi kamwe kuandika tena. Unarudia tena kumwambia Baruku maneno yote ya kitabu kile. Lakini wakati huu unaongeza ujumbe zaidi.

Ujumbe ambao unawapelekea watu ni ule ule tu. Unawataka wafahamu kwamba Mungu anawapenda watu wake na ataendelea tu kuwapenda. Nawe unawaandikia hivi, "Tutaadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu na nchi yetu itaangamizwa lakini kunalo tumaini. Siku moja Mungu atawarudisha watu pamoja ili waabudu tena hapa Yerusalemu."

Muda si muda, jeshi la Wakaldayo linavamia mji wenu. Kuta zote zinabomolewa, nyumba zinachomwa nalo Hekalu linaharibiwa vibaya sana. Watu wanalazimishwa watembee kwa mistari mirefu hadi Babeli. Wewe mwenyewe unaanza kulia. Wanajeshi wa Wakaldayo wanakwambia uchague iwapo unataka kwenda Babeli au unataka kubaki Yuda. Nawe unaamua kubaki pamoja na wale walioachwa. Baadaye unalazimishwa kwenda Misri.

Unaendelea kunena ujumbe wa Mungu kwa miaka arobaini na mmoja. Nao watu wako wanashindwa kukuelewa kwa hivyo wanakwita msaliti. Unapigwa na kufungwa gereza. Hata unatamani kufa, lakini hukati tamaa. Hatimaye unajifunza kwamba Mungu anawatumia watu wa mataifa ili kutimiza mipango yake.

KAZI YA KUFANYA

Unayo maswali yanayohusu Yeremia. Hebu jifanye kama kwamba unamwandikia barua. Baadaye uandike majibu ambayo unadhani Yeremia atasema katika mwisho wa barua hiyo.

Kwa Rafiki Mpendwa, Yeremia,

Tafadhali, unaweza kujibu maswali yafuatayo?

1. Je! Baba yako aliitwaje?
2. Je! Ulikuwa ukiishi wapi?
3. Je! Ni kisingizio gani ulichomtolea Mungu alipokwambia kwamba ana kazi ya wewe kumfanyia?
4. Je! Mungu Alikuahidije?

Asante kwa kunisaidia ili nikufahamu vizuri.

Ni Mimi

Rafiki yako

Tafuta majibu ya maswali haya kutoka kwa maandiko ya Biblia na uyaandike.

1. (Yeremia 1:1) _____
2. (Yeremia 1:1) _____
3. (Yeremia 1:6) _____
4. (Yeremia 1:8) _____

Mungu alisema na Yeremia na akamfundisha jambo muhimu akiwa nyumbani kwa mfinyanzi. Soma Yeremia 18:1-6 na ujibu maswali haya yahasuyo yale aliyooona.

1. Je! Yeremia aliona nini nyumbani kwa mfinyanzi (Kifungu cha 3)

2. Je! Nini kilichofanyika kwa chombo ambacho mfinyanzi alikuwa akikitengeneza? (kifungu cha 4)

3. Je! Mfinyanzi alikifanyaje kile chombo kilichoharibika? (kifungu cha 4)


4. Je! Yeremia alijifunza nini kutokana na jambo hili? (kifungu cha 6)

Kuna funzo pia ambalo nasi twapaswa kujifunza. Yule mfinyanzi angeweza kuuponda au kuutengeneza upya. Aliamua kukifinyanga upya kulingana na vile anavyotaka mwenyewe.

Mungu ni mfinyanzi wa maisha yetu. Anatutaka tumwitikie jinsi udongo ulivyo mikononi mwa mfinyanzi. Ni lazima tubadilishwe wakati tunapokuwa kama udongo unaoasi. Mungu ni pendo. Yeye ni mfinyanzi mvumilivu ambaye hutusamehe na kutufanya upya ili tuwe kama Yesu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Angalieni, kama udongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi, ndivyo mlivyo ninyi katika mkono wangu, Ee nyumba ya Israeli” (Yeremia 18:6b)



Udongo ambao ni majimaji si mzuri. Hata hupendezwi kutazama magurudumu ya mfinyanzi. Hali, wakati mfinyanzi anaanza kufinyanga udongo ule huanza kuonekana kama chombo fulani. Hata huweza kutengeneza chombo kizuri na cha kupendeza kutoka kwa udongo huo.

Mungu yuko tayari kutufanyia tuwe wa manufaa na wakupendeza machoni pake. Lakini ni lazima tuwe tayari kumwacha atufanyia jinsi atakavyo. Taja jambo moja ambalo Mungu anataka kukufanyia maishani mwako ili akuwezeshe kuwa kama Yesu.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps


© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA KUMI NA MOJA

SWALI LA MALAKI: "JE! MWANADAMU ATAMWIBIA MUNGU?"

MASOMO YA BIBLIA: Malaki 3:6-12

Mwalimu wa Shule ya Jumapili aitwaye Bw. Banda, alimkuta Chege akiwa darasani alipofika huko wakati wa Jumapili asubuhi. Chege alikuwa ameshika Biblia mikononi mwake akiwa anaisoma.



Bw. Banda: Chege, unafanya nini?

Chege: Najaribu kutafuta kitabu cha Malaki katika Biblia. Je! kiko wapi?

Bw. Banda: Malaki ni kitabu cha mwisho katika Agano la Kale. Kiko mbele ya Injili ya Mathayo. Kwa nini unatafuta kitabu cha Malaki?

Chege: Unakumbuka kwamba Jumapili iliyopita Mchungaji Sole alihubiri juu ya kumwibia Mungu na akasoma Maandiko kutoka katika

kitabu cha Malaki. Nimefikiria sana juu ya jambo hili kwa wiki nzima. Ikiwa vitu vyote ni mali ya Mungu, Je! inawezekanaje mwanadamu kumwibia Mungu?

Bw. Banda: Chege, jambo hili lawezekana. Je! Unakumbuka jinsi Mchungaji Sole alivyosema tunaweza kumwibia Mungu?

Chege: Alisema kwamba kwa kutotoa zaka wala sadaka. Lakini sielewi maana ya kutoa zaka na sadaka. Je! Unaweza ukanisaidia ili nijue ni nini?

Bw. Banda: Neno hili "zaka", linamaanisha sehemu moja ya kumi. Historia inaonyesha watu wa Ashuru, Roma, Misri, Babeli na Wakaldayo walikuwa wakiitolea miungu yao zaka, miaka mingi sana kabla ya kuzaliwa kwa Yesu.

Chege: Je! Walikuwa na pesa siku hizo?

Bw. Banda: Siku hizo hawakuwa wakitumia pesa, lakini walitoa zaka ya mali waliyokuwa nayo. Kwa mfano, waliweza kutoa fungu la kumi la

mavuno waliyovuna kama tendo la kurudisha shukrani.

Chege: Je! Kwa nini basi tunapaswa kutoa zaka iwapo ilianza kwa ibada za miungu?

Bw. Banda: Jambo hili lilianza wakati wa Agano la Kale kama tendo la kumrudishia shukrani Mungu wa kweli. Ibrahimu ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kutoa zaka. Baadaye tunaona kwamba Yakobo aliahidi kutoa zaka mali yote ambayo alipewa na Mungu. Naye Mungu alimpa Musa amri zihusuzo utoaji wa zaka zilipaswa kutiiwa na wana wa Waisraeli. Kumbuka kwamba walitoa zaka ya mali waliyonayo. Kutoka kwa mazao, ng'ombe, kondoo na mbuzi.

Chege: Je! ni nani aliyeipokea zaka hii?

Bw. Banda: Zaka hii ilikuwa kuwasaidia wale waliokuwa watumishi wa sanduku la Agano, na baadaye ikawa inapewa wale waliohudumia Hekalu.

Chege: Je! Watu wa Mungu walitii na kutoa kila mara zaka ya mali zao?

Bw. Banda: La, na hii ndiyo sababu iliyomfanya Nabii Malaki kuandika juu ya zaka. Mungu alikuwa ametoa sheria za kuwakumbusha kwamba yeye ndiye mtoaji na mmilikaji wa vitu vyote. Lakini Wayahudi walitotii amri hizi za Mungu na wakakosa baraka za Mungu. Soma Malaki 3:6-12 na halafu tuzungumzie juu ya maana ya vifungu hivi. ("Chege, hebu soma vifungu hivi kutoka kwa Biblia.")

Bw. Banda: Malaki aliandika ujumbe wake kama kwamba Mungu ndiye aliyekuwa akiongea na watu. Alianza kwa kuwakumbusha yeye habadiliki. Miaka mingi ilikuwa imepita tangu

Mungu alipompa Musa amri zake, lakini yeye aliwatarajia Wayahudi kutii yote ambayo waliambiwa.

Chege: Kifungu cha 8 kinazungumzia zaka na sadaka. Je! Hii inamaanisha kwamba watu walipaswa kutoa zaidi ya zaka?

Bw. Banda: Hasa Mungu alihitaji zaka. Nao watu hawangeweza kuiepuka. Hata hivyo, Mungu alifurahi pia iwapo walimtolea hata sadaka. Hii ilitolewa zaidi ya zaka. Mungu aliwaahidi baraka kwa sababu ya utiifu wao.



Chege: Je! Inamaanisha nini kusema kwamba leteni zaka kamili ghalani? Je! Ghala yenyewe ikowapi?

Bw. Banda: Walipaswa kuleta zaka Hekaluni ambako ndiko zilikowekwa na kutumiwa wakati zilipohitajika. Hii ndiyo sababu kifungu cha 10 kinaendelea kwa kusema kwamba, "...ili kuweko chakula katika nyumba yangu..." Wale waliohudumia hekaluni walipaswa wapate riziki yao kutoka kwa mali zilizotolewa na watu.

Chege: Sijawahi kufikiria kwamba kuna madirisha mbinguni, lakini kifungu cha 10 kinasema kwamba kunayo madirisha.

Bw. Banda: Mungu alikuwa akisema kwamba angewaminia baraka nyingi. Watu wangeweza kuthibitisha uaminifu wa Mungu iwapo wanuia kumjaribu. Mungu aliwatajia baadhi ya baraka ambazo zingekuwa zao. Wadudu hawangeharibu mazao yao, kungekuwa na mazao mengi ya matunda yao. Hii inaonyesha kwamba angewaitea mvua ili wapate mavuno mengi. Hata nao jirani zao wangewaita waliobarikiwa.

Chege: Je! Mungu yungali anatutaka sasa tutoe zaka na sadaka?

Bw. Banda: Chege, nimefurahi kwamba umeuliza swali hilo. Watu wa Mungu siku hizi hawaishi kwa amri zile zile zilizokuwa za Agano la Kale. Hata hivyo, Mkristo hapaswi kutoa mali ndogo chini ya neema za Mungu kuliko vile Wayahudi walitoa kulingana na amri walizopewa. Zaka na sadaka tunazotoa ni dhihirisho la nje linaloonyesha jinsi tulivyojitoe kwa Mungu.

Chege: Siku hizi hatuna sanduku la Agano au Hekalu. Je! Zaka na sadaka zinatumiwaje kanisani mwetu?

Bw. Banda: Je! umewahi kufikiria mahali ambapo mchungaji Sole hupata pesa za kuilishia jamaa yake?

Chege: Bado.

Bw. Banda: Yeye hulipwa kutokana na zaka na sadaka tunazotoa kila Jumapili. Pesa hizo pia hutumiwa kwa kununua vitabu vya nyimbo, vitabu vya Shule ya Jumapili, vifaa vya kusafishia na kufagia kanisa na baadhi yazo

kutumiwa kwa kumsaidia Mchungaji wa kanisa jipya lililoanzishwa.

Chege: Asante sana Bwana Banda, sasa mimi sipati pesa, Je! Nitawezaje kutoa zaka?

Bw. Banda: Ni vigumu sana kwako kupata pesa za kutoa zaka wakati ungaliko shuleni. Siku inakuja ambapo utaweza kutoa. Hata hivyo, sasa ndio wakati wako mzuri wa kujitoe kwa kutoa zaka ya yale yote ambayo Mungu amekuwezesha kupata. Ukianza sasa kutoa zaka wakati una mali chache, itakuwa rahisi kwako kutoa wakati una mali nyingi.

Chege: Lakini nataka kusaidia kwa sasa. Je! Nitafanyaje?

Bw. Banda: Wiki iliyopita uliniambia kwamba unataka uanze kulima shamba. Unaweza kutoa fungu la kumi kutokana na pesa ambazo utapata baada ya kuuza mazao yako. Kumbuka pia kumtolea Mungu sehemu yake wakati mtu anapokwajiri kazi ya muda na kukulipa.

Chege, ni kweli kwamba mtu hawezi kutoa zaidi ya Mungu. Lakini hasa baraka za Mungu kwa watoto wake zaweza kuwa ni mali, lakini jambo la muhimu sana ni kwamba, yeye hutupa rehema zake, amani na upendo.

Chege: Sitaki kuwa na hatia ya kumwibia Mungu, kwa hivyo ninauhakika kwamba atanisaidia kujua kitu cha kutoa. Nataka nitoe hata na sadaka.

Bw. Banda: Nitapendelea wakati mwingine tuzungumze juu mambo mengine ya kumwibia Mungu mali na zaka na sadaka. Mungu anatutaka tutumie vyema vitu vyote alivyotupatia.

Hii ni pamoja na miili yetu, muda, vipawa na hata maongozi yetu. Tutajadiliana juu ya mambo haya baadaye. Kwa sasa tunapaswa tuanze kuwakaribisha washiriki wenzetu wa darasa letu na tuanze somo letu la leo.

KAZI YA KUFANYA

1. Soma Malaki 3:6-9 na uweke alama hii (✓) kando ya sentensi iliyo kweli.

_____ Bwana habadiliki.

_____ Wayahudi walikuwa waaminifu katika kutii amri za Mungu.

_____ Wayahudi walikuwa wamekosa kumtii Mungu kwa muda Mrefu.

_____ Mungu hangewaadhibu kamwe Wayahudi kwa sababu alikuwa anawapenda.

_____ Watu walimwibia Mungu zaka na sadaka.

_____ Taifa lote walitotii Mungu.

2. Soma Malaki 3:8-12 na ujaze nafasi zilizoachwa.

Mungu alisema kwamba watu walikuwa wamwibia z_____ na s_____. Jambo hili lingelifanya taifa lote lipate l_____. Mungu angewamwagia b_____ iwapo watu wangetubu na kuleta zaka zao kamili katika _____. Mungu naye hangewaacha wadudu waharibu m_____ ya arthi yao. Mataifa mengine yangeweza kuona jinsi wanavyopendeza na kuwaita wenye h_____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la” (Malaki 3:10).

Kifungu chetu cha kukumbuka ni amri iliyo na kusudi. Kungekuwa na mali ya kutosha kuendeleza kazi ya Mungu iwapo watu wangetoa zaka na sadaka zao. Nao watu wa Mungu wangemwagiwa baraka.

3. Andika katika nafasi ifuatayo ili AMRI na AHADI iliyotolewa katika kifungu cha 10.

Amri ya Mungu (kifungu cha 10a) _____

Ahadi ya Mungu (kifungu cha 10b) _____

4. Je! Utajitoa na kumtolea Mungu ahadi ya kumpa zaka na sadaka yako kupitia kwa kanisa lako? Amri na ahadi ya Mungu inakuhusu hata wewe.

AHADI YANGU YA KUTOA ZAKA

Nimetambua kwamba vyote nilivyonavyo na vile ambavyo nitakuwanavyo vinatoka kwa Mungu. Kwa hivyo ninaahidi kumtolea zaka ya mali yote ambayo ananibariki nayo.

Weka sahihi _____



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA TATU **KITABU CHA PILI**

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA KUMI NA MBILI
MUNGU ANAWAPENDA WATU WOTE

MASOMO YA BIBLIA: Yona 1:1-3;
3:1-3; 4:1-6

Umati wa washiriki waligeuka na kuwaangalia wageni waliokuwa wakiingia kanisani. Walikuwa wamevalia mavazi tofauti sana kulingana na wale watu waliokuwa wamekaa kanisani.

Mercy alimgeukia rafiki yake, Ona, na akamwuliza, "Je! hawa ni akina nani? Kwa nini wamekuja hapa? Je! Hawajui kwamba hawajakaribishwa kanisani kwetu? Ona kamwambia, "Ni lazima tuchunge sana vitabu vya nyimbo. Nimesikia kwamba watu wa kabila hili ni wezi sana."

Wasichana hawa waliendelea tu kunong'onezana wakati mchungaji alipokuwa anahubiri. Baadhi yao waliandika habari kuhusu wageni hawa wa ajabu.

Wakati washiriki walipokuwa wakiimba wimbo wa mwisho, mmoja kati ya wageni hawa alienda mbele ya kanisa. Mchungaji aliongea na kijana huyu na wote wakapiga magoti ili waombe.

Mwishowe mchungaji alisema kwamba, "Kijana huyu amekuja mbele kwa sababu amesikia kwamba Mungu anampenda. Amemwomba Mungu amsamehe dhambi zake na awe pia Bwana na Mwokozi wake.

Vijana wengine wote waliangaliana. Hawakujua jambo la kusema. Je! Wewe ungesemaje iwapo jambo hili lilikuwa kanisani mwako? Andika jibu lako katika nafasi ifuatayo.

Somo letu la leo linahusu nabii aitwaye Yona. Mungu alimtuma kwenda na kuwahubiria watu wa Ninawi, watu ambao Yona hakuwapenda. Wao walikuwa watu wa Mataifa na Yona alikuwa Myahudi. Mungu alimwonyesha Yona kwamba alikuwa akiwapenda watu wote, Wayahudi na watu wa Mataifa.

Ninawi ulikuwa mji mkuu wa nchi ya Ashuru. Mungu hakupendezwa na uabuduji wake wa sanamu na jinsi walivyoyatendea mataifa yaliyokuwa dhifu.

Mungu alimwambia Yona awaonye watu wa Ninawi kwamba ataangamiza iwapo hawataacha uovu wao. Yona alisikia neno la Mungu alioambiwa lakini hakutaka kulitii. Hakutaka kuwatolea ujumbe wa Mungu watu ambao hawapendi. Yona alijaribu kumkimbia Mungu. Alienda katika bandari ya Yafa na akaipanda merekebu ambayo ilikuwa ikienda upande tofauti na Ninawi.

Kulitokea dhoruba kuu baharini baada ya wao kusafiri kwa muda kidogo tu. Wale mabaharia waliogopa sana na wakaanza kumwomba Mungu wao ili awasaidie. Walitupa mizigo yao baharini ili merekebu yao isizame baharini.

Yona alikuwa amelala usingizi katika upande wa ndani za merekebu hiyo wakati dhoruba ilipoanza. Nahodha alimwendea na akamwuliza, "Je! Mbona unalala wakati kama huu? Amka na umwombe Mungu wako ili atusaidie."

Wale wasafiri walianza kuulizana maswali ili kuona ni yupi kati yao aliyeanzisha mkosi wa dhoruba. Walipiga kura, na kura hizo zikawa kwa Yona.

Yona alikubali kwamba yeye ndiye aliyesababisha dhoruba hiyo. Akawaambia, "Mimi ni mwebrania; nami namcha Bwana, Mungu wa mbinguni." Sasa, alimkimbia Mungu Aliwaambia mabaharia hao kwamba dhoruba ingetulia iwapo wangemtupa



baharini. Walifanya jinsi Yona alivyowaambia nayo habari ikatulia.

Mungu alikuwa akimtayarisha samaki mkubwa wa kummeza Yona. Alikaa tumboni mwa samaki kwa muda wa siku tatu, usiku na mchana. Aliweza kutubu na kumwomba kwa kutotii kwake alipokuwa tumboni mwa samaki. Samaki huyo aliweza kumtapika Yona pwani ilipofika siku ya tatu.

Mungu aliweza kusema tena na Yona. Akamwambia, "Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukaihubiri habari nitakayokuamuru?" (Yona 3:2)

Yona aliweza kwenda Ninawi wakati huu. Alipofika huko, aliwahubiria watu ujumbe wa kuwaonya. Aliwaambia kwamba Mungu angeuharibu mji wao kwa muda wa siku arobaini. Watu wa Ninawi walimwamini na wakatubu dhambi zao. Hata mfalme aliamini

kwamba ujumbe wa Yona ulikuwa umetoka kwa Mungu.

Mungu hakuuharibu mji huo alipoona kwamba watu wa Ninawi walikuwa wametubu kwa moyo wa kweli. Yona alikasirika sana. Alikuwa amefanya jinsi Mungu alivyomtaka afanye, lakini hakuwa akitaka moyoni mwake kuona watu wakiabudu Mungu. Wao walikuwa wametubu, lakini Yona hakumtaka Mungu awasamehe. Yona alitoka mjini humo. Akajifanyia kibanda, halafu akakaa chini ya uvuli wake na kungojea kuona kile kitakachotokea huko.



Mungu aliufanya mtango ukue ili Yona akae chini ya kivuli chake. Lakini pia Mungu alimtayarisha buu wa kuweza kuula mti huo. Mti ule ulinyauka na kukauka. Upepo mkali wa kutoka mashariki ulianza kuvuma, nalo jua likawa kali. Yona alidhania kwamba atazimia, na akamwambia Mungu ni afadhali afe.

Mungu akamwambia Yona, “Je! Unatenda mema kukasirika kwa ajili ya mtango? Wewe hukuupanda wala kuukuza mtango huu. Nawe umeuhurumia mtango huu, lakini hujawahurumia watu ambao wanakufa katika mji huu mkubwa. Kuna watu zaidi ya mia na ishirini elfu ambao wangali wanaishi gizani.

Ujumbe wa Mungu ni wa kila kabila na nchi hapa duniani. Anataka ujumbe wa upendo na wokovu uhubiriwe kwa watu wote po pote walipo. Je! Ukotayari kuwashuhudia watu ambao wanaishi maisha tofauti na yako? Je! Utawaambia kwamba Mungu anawapenda na alimtuma Yesu kufa kwa ajili ya dhambi zao pia?

KAZI YA KUFANYA

Soma kila sentensi ifuatayo, na ujaze kwa neno lililosahihi katika nafasi iliyoachwa. Maneno yenyewe yameandikwa chini ya sentensi hizi.

1. Mungu alimwambia Yona aende _____
2. Yona alienda katika bandari ya Yafa na akapata merikebu ikiwa inaenda _____
3. Alipokuwa kwenye merikebu ili kulitokea _____ kuu.
4. Mabaharia walimtupa Yona baharini. Mungu alikuwa amemtayarisha _____ mkubwa ili ameze Yona.
5. Yona alikuwa ndani ya tumbo la samaki kwa muda wa _____ mchana na usiku.
6. Yona _____ wakati alipokuwa tumboni mwa samaki.
7. Yona alihubiri ujumbe ambao Mungu alikuwa amempa, alipofika

Ninawi. Aliwaonya kwamba Mungu angeuangamiza mji wa Ninawi baada ya siku _____

8. Watu _____ waliposikia ujumbe wa Mungu.
9. Mungu _____ mji huo kwa sababu ya kutubu kwao.

Maneno: Ninawi, siku tatu, walitubu, Tarshishi, arobaini, dhoruba, alitubu, samaki, hakuuangamiza.

Soma Yona 4:1-4, na uchore mvingo kwenye jibu sawa la maswali yafuatayo:

1. Je! Kwa nini Yona alikasirika?
 - a. Yule samaki mkuu alitoweka.
 - b. Mungu alikuwa amem-danganya.
 - c. Watu wa Ninawi walitubu.
2. Je! Yona alimwambiaje Mungu?
 - a. Umebadili nia yako.
 - b. Wewe ni Mungu mwenye mapenzi na rehema.
 - c. Unawapenda tu Waisraeli.
3. Je! Mungu alimjibuje Yona?
 - a. Waweza kufa ukitaka.
 - b. Mimi nakupenda. Tafadhali usikasirike.
 - c. Je! Unatenda vema kukasirika?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa maana sionei haya Injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia" (Warumi 1:6).

Yona aliwakasirikia watu wa Ninawi. Hakuwataka wapate nafasi ya kumwabudu Mungu jinsi ilivyo kuwa Wayahudi.

Kuna orodha ya watu tofauti hapa chini. Wapange kuanzia mtu wa kwanza hadi wa kumi. Mfanye mtu wa 1 awe yule ambaye unaweza kumpenda kwa urahisi. Na yule wa 10 awe mtu ambaye unapata shida ya kumpenda. Andika sasa namba yako jinsi zinavyofuatana:

- _____binamu yako (mtoto wa ndugu ya baba au mama)
- _____mtu wa kabila lingine
- _____mtu wa kutoka nchi nyingine ya Afrika
- _____kilema
- _____mfungwa
- _____mzee
- _____mtoto wa mtawala
- _____mwana michezo hodari
- _____askari au polisi

Je! unafikiri kwamba Mungu anapenda watu fulani kuliko wengine? Weka alama hii (✓) kwenye jibu lako. () Ndiyo () La.

Yona alijifunza kwamba Mungu anawapenda watu wote. Jaribu wiki hii kumwambia mtu wa kabila lingine juu ya upendo wa Yesu Kristo. Mwambie kwamba Mungu anampenda na hata wewe unampenda pia.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA TATU KITABU CHA PILI

HABARI ZA MANABII

J3 - 2Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

SURA YA KUMI NA TATU

KUWA NA UJASIRI WAKATI WA HATARI

MASOMO YA BIBLIA: Danieli 6:7, 10-11, 16-23

Danieli alikuwa nabii aliyeamini kwamba Mungu angemsaidia wakati wa shida. Alijua jinsi ya kuomba, na alipata nguvu za Mungu alipoomba wakati wa shida. Yeye ni mmojawapo wa watu wenye ujasiri sana tunaofunza habari zao kutoka kwa Agano la Kale.

Danieli alishikwa na kupelekwa katika gereza la Babeli alipokuwa yungali kijana. Mfalme wa Yuda, Nebukadneza, alisema kwamba alitaka vijana wa Kiyahudi walioshikwa kufundishwa lugha na desturi za Wababeli.

Alisema pia kwamba wanapaswa kulishwa chakula bora na kunywa divai ya mfalme. Danieli na rafiki zake watatu walikataa kula chakula walichotayarishiwa na mtumishi wa Mfalme. Badala yake walitaka wapewe mboga na maji ya kunywa.

Danieli na rafiki zake waliweza kuwa na nguvu nyingi kuliko vijana wengine



wo wote, kwa sababu ya chakula walichokula.

Baada ya muda kidogo kupita, Babeli ilipata mfalme mpya aitwaye Dario, ambaye alikuwa Mmedi. Kwa sasa, hebu tujifanye kama kwamba Danieli anatusimulia hadithi yake mwenyewe.

“Wakati Dario alipofanywa mfalme wa Babeli, aliigawa nchi hii katika sehemu nyingi mbalimbali. Kulikuwa na kiongozi au liwali aliyesimamia kila sehemu. Kila liwali alikuwa chini ya mmojawapo wa watawala watatu waliochaguliwa na Dario. Mimi nilikuwa mtawala kwa muda. Hatimaye, Mfalme Dario alinichagua niwe juu ya kila kitu katika ufalme wake.

“Huu ulikuwa wajibu mkubwa sana na nilifanya kazi zangu kwa uaminifu na kwa haki. Watu wengi walinionea wivu kwa sababu ya cheo changu. Walijaribu kutafuta makosa katika mambo niliyofanya, ili niondolewe kwenye cheo changu. Hawakupata ubaya wo wote na kazi yangu, kwa hivyo walianza kulaumu ibada ninazofanya kwa Mungu.

“Wale maliwali walionipinga walijua kwamba ninaomba mara tatu kwa siku. Walitumia jambo hili kwa kumfanya mfalme apitishe amri ambao ingenidhuru. Amri hii ilisema kwamba mtu ye yote atakayemwomba mungu mwengine isipokuwa mfalme kwa muda wa siku thelathini, atakupwa kwenye tundu la simba. Walimwambia mfalme aweke sahihi yake naye akaweka sahihi.

“Mimi niliamua kuendelea na maombi yangu kwa sababu nilijua kwamba ilikuwa vyema kufanya hivyo. Viongozi wa serikali walinichunguza ili waone kile nitakachofanya. Walienda kumwambia mfalme waliponiona nikiomba karibu na dirisha langu. Wakamwambia, ‘Je! Hukutia sahihi kwa amri isemayo kwamba mtu ye yote asimwombe mtu mwingine isipokuwa



wewe tu kwa muda wa siku thelathini? Tumemwona Danieli akimwomba Mungu wake mara tatu kwa siku, kwa hivyo, ni lazima atupwe kwenye tundu la simba.

“Sheria haingewezwa kubadilishwa baada ya kupitishwa. Mfalme Dario alijua kwamba hangeweza kamwe kufanya lo lote. Alihuzunika sana. Mfalme alikuwa akinipenda naye alijaribu kufikiria jinsi awezavyo kuniokoa, lakini hakuweza kufanikiwa.

“Mfalme aliwaamuru watu wake kunishika na kunitupa katika tundu la simba. Akaniambia, ‘Mungu wako unaye mtumikia daima, yeye atakuponya.’ Ni ajabu ilioje! Mfalme Dario hakuweza kulala usiku kucha. Alikataa kula cho chote. Alihuzunika sana kwa sababu alikuwa ame-danganywa na kutia sahihi kwenye sheria hiyo.

“Sasa tunaelekea kwenye sehemu ya kuşisimua sana. Nilikuwa mtawala wa serikali, lakini sikuwa na matumaini niliposukumwa kwenye tundu lile na kufunikwa na jiwe kubwa. Kwanza kabisa sikuweza kuona kwa sababu kulikuwa na giza kuu humo. Hatimaye, macho yangu yalianza kuona vizuri. Niligundua kwamba malaika alikuwa akifunga kinywa cha simba. Mungu alikuwa akinilinda kutokana na wale ambao walitaka kuniua.

Mfalme alikuja asubuhi na mapema pale nilipokuwa tunduni. Naye akanililia kwa sauti ya huzuni, “Danieli, Je! Mungu ameweza kukuponya kutokana na simba hawa?

“Nilifurahi kumwambia kwamba Mungu alikuwa ameniponya kwa kumtuma malaika aliyefunga vinywa vya simba hao, hata hawakupata kunidhuru.

“Mfalme aliwaamuru tena watu wake wanitoe kutoka kwenye tundu lile la simba. Aliona kwamba sikuwa nimudhuriwa kwa sababu nilimwamini Mungu. Hatimaye alipitisha tena sheria nyingine. Sheria hii ilisema kwamba kila mmoja katika ufalme wake anapaswa kumwabudu Mungu yule ambaye ninamhudumia.

“Nimewasimulia hadithi yangu hii kwa sababu nataka iwe mfano kwetu. Niliweza kuwa na nguvu kwa sababu nilimwamini Mungu, wala sio katika nguvu zangu mwenyewe. Mungu alijua kwamba sikuwa na hatia ya kosa lo lote. Nilikuwa mwaminifu kwake, naye alinisaidia wakati wa shida.

Je! Unewahi kutomtii Mungu kwa sababu uliogopa yale ambayo ungeambiwa na rafiki zako? Je!

Umewahi kuona haya kuomba mbele ya rafiki zako ambao si Wakristo? Danieli alikuwa na ujasiri kwa sababu alimwamini Mungu hata alipapaswa kufa.

Je! Danieli alipataje ujasiri? Ni kwa sababu alikuwa na uhusiano mzuri na Mungu. Alikuwa amejizoesha kumwomba Mungu mara tatu kwa siku. Danieli aliweza kusimama imara kwa Mungu alipopatwa na shida. Alikuwa tayari kufa badala ya kutomtii Mungu.

Je! uko tayari kuwa kama Danieli? Unapaswa kuwa kama Danieli iwapo unataka kusimama imara. Inapaswa kuwa Danieli wakati wanafunzi wenzako wanapoanza kukuchekelea na kukulaumu kwa sababu u Mkristo Pengine dada au ndugu zako hukuchekelea wakati unaposoma Biblia na kuomba, hata hivyo, unapaswa uwe Danieli.

KAZI YA KUFANYA

Soma Maandiko uliyopewa na ujibu maswali hayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa.

1. Danieli 6:7. Je! Ni sheria ipi ambayo mfalme alitia sahihi? “...mtu ye yote _____ dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku _____, ila kwako, Ee _____, _____ katika _____ la _____.”
2. Danieli 6:10. Je! Danieli alifanyaje aliposikia habari za sheria hii? Danieli aliingia _____ mwake akapiga _____ mara _____ kila siku na kusali.
3. Danieli 6:14. Je! Mfalme alijisikiaje

alipoambiwa kwamba Danieli alikuwa amevunja sheria hii? _____

4. Danieli 6:18. Je! Mfalme alifanyaje kuonyesha kwamba alihuzunika sana wakati Danieli alipotupwa kwenye tundu la simba?

Alienda _____ kwake, akakesha usiku kucha, _____ wala hakupata _____.

5. Danieli 6:19-20. Je! Mfalme alifanya nini kulipokuwa asubuhi na mapema?

Alienda kwa haraka mpaka kwenye lile _____ la _____ na akamlilia Danieli akisema, "Ee Danieli mtumishi wa _____ aliye hai, Je! _____ wako unayemtumikia daima, ameweza _____ na _____ hawa?"

6. Danieli 6:23b. Je! Kwa nini Danieli hakudhuriwa?

Ndipo Danieli alipotolewa katika lile tundu wala _____ lo lote halikuonekana mwilini mwake, kwa sababu alikuwa _____ wake.

Andika sentensi zifuatazo kulingana na vile zilivyofanyika. Andika namba 1 kuanzia lile lililofanyika kwanza, na namba 2 kwa lile lililofuatia na uendelee vivyo hivyo hadi mwisho. Umejaziwa nafasi ya jibu la kwanza.

_____ Danieli na rafiki zake watatu walikataa kula chakula cha mfalme.

_____ Danieli alitupwa kwenye tundu la simba.

1 Danieli alipelekwa Babeli kama mfungwa.

_____ Watawala wa mfalme walimpata Danieli akiomba.

_____ Danieli alikuwa mmojawapo wa watawala wa Mfalme Dario.

_____ Mfalme alipitisha sheria kwamba kila mtu atapaswa kumwabudu Mungu wa kweli.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Bwana ni nuru-yangu na wokovu wangu, Nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, Nimhofu nani" (Zaburi 27:1).

Taja jambo moja linalokufanya uogope. _____

Omba kwa kutumia kifungu cha kukumbuka ukimwambia Mungu kwamba, "Wewe, Bwana ni ngome ya uzima wangu, sitaweza kuogopa _____."

(andika kile ambacho unakiogopa)

Danieli alikuwa na ujasiri kwa sababu alimwamini Bwana. Je! Wewe unamwamini Bwana? Unapaswa uwe kama Danieli.